SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Wananchi** wawashtaki wauguzi na madaktari kwa Mkuu wa Mkoa

UKURASA 2




Nipashe Jumapili
MWANGA WA JAMII
Jumapili Aprili 17, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580918
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# CAG abaini tatizo ujenzi wa hoteli ya Burigi Chato

• **Ni** ya nyota tatu iliyogharimu bilioni 11/-, hali mbaya yaibuliwa ndani ya magereza... *Endelea ukurasa 2 & 3*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### WIZARA YATOA KIBALI CHA AJIRA 1,650 AFYA

SERIKALI imetoa kibali cha ajira za watumishi 1,650 wa kada mbalimbali za afya, ambao wataajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi vilivyoko chini ya Wizara ya Afya...




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akifungua kongamano la pili la madaktari na wahudumu wa afya, lililoandaliwa na Taasisi ya Jamiyyatul Akhlaqul Islaamia (JAI), jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

## Mkandarasi apewa zabuni, aiuza kisiri kwingine na kujipatia mabilioni

UKURASA 3

## Askofu akemea matatizo ya wananchi kuwa mtaji, fursa

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA SC KAZI MOJA TU LEO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Mbunge wa Jimbo la Ruangwa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akipiga kura kuwachagua viongozi wa shina namba moja, Tawi la Nanguruwe, katika uchaguzi uliofanyika Kata ya Nandagala, Ruangwa, mkoani Lindi jana. Chama hicho, kipo katika hatua za kufanya chaguzi za ndani kwa ngazi zote. **PICHA: OWM**

# CAG abaini tatizo ujenzi hoteli ya Burigi Chato

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini upungufu katika mradi wa ujenzi wa Hoteli ya Burigi Chato yenye hadhi ya nyota tatu wa thamani ya Sh. bilioni 11.04.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumanne ya wiki hii, CAG anabainisha kuwa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) liliingia mkataba na kampuni ya ujenzi ya SUMA JKT kwa ajili ya ujenzi wa hoteli hiyo Aprili 4, 2020 na kazi ilitakiwa kukamilika Aprili 14, 2021.

Anasema mapitio yake ya taarifa za maendeleo ya mkataba wa ujenzi wa Hoteli ya Burigi Chato yalibaini upungufu kadhaa, ikiwa ni pamoja na TANAPA kutoa malipo ya awali ya Sh. bilioni moja bila kuwa na mchanganuo wa gharama za ujenzi kama msingi wa kukokotolea malipo ya awali.

Vilevile, CAG anasema ujenzi wa hoteli ulianza bila kufanya tathimini ya athari ya mazingira ambayo ni muhimu ili kuepuka uharibifu wa mazingira.

"Pia kulikuwa na ucheleweshaji wa kukamilika kwa kazi kwani mradi ulipangwa kukamilika tarehe 14 Aprili 2021 lakini ujenzi ulikuwa upo katika hatua ya awali ya msingi hadi Julai 2021.

"Taarifa za ujenzi zilionyesha ucheleweshaji huo ulitokana na mkandarasi kuwa na vifaa vichache kwenye eneo la ujenzi, ambavyo baadhi vilikuwa havifanyi kazi na kusababisha ucheleweshaji.

"Kwa maoni yangu, kukosekana kwa taratibu sahihi za ununuzi kulisababisha TANAPA kushindwa kukamilisha mradi kwa wakati, jambo ambalo linaweza kusababisha gharama za ziada kutokana na kuongezeka kwa bei za vifaa.

"Ninapendekeza Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania lihakikishe lina mikakati ya kuwezesha mradi kukamilika bila kuchelewa zaidi," CAG anatoa hoja.

# Askofu akemea viongozi, matajiri kufanya matatizo ya wananchi fursa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Katoliki Jimbo Kuu la Songea, Damian Dallu, amewashukia baadhi ya viongozi wa serikali na wafanyabiashara wanaotumia matatizo ya wananchi kama fursa kujineemesha wakati huu wa hali mbaya ya kiuchumi.

Askofu Mkuu Dallu alitoa kauli hiyo juzi wakati wa mahubiri ya ibada ya Ijumaa Kuu katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Mathias Kalemba, mjini hapa iliyoshirikisha waumini wa dini ya Kikristo. Ibada hiyo ilikuwa ya kukumbuka kuteswa na kufa kwa Mwokozi Yesu Kristo yapata miaka 2,000 iliyopita.

Wakati wa mahubiri hayo, Askofu Mkuu Dallu alisema kitendo cha baadhi ya watu wenye mamlaka pamoja na wafanyabiashara kutumia matatizo ya watu na kugeuza kuwa fursa kwao ni kibaya na si jambo la kufurahisha.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wanaojihusisha na kujineemesha kwa matatizo na shida za wananchi, kuacha mara moja na badala yake watende haki kwa kila mwananchi.

Askofu Dallu alisema Yuda Iskariote alimsaliti Yesu Kristo lakini katika nyakati zetu hizi kina Yuda wamekuwa wengi jambo ambalo linasababisha kutokuona shida na matatizo ya wengine. "Kila mwananchi kwa nafsi aliyo nayo anapaswa kujihoji na kubadili tabia mbaya aliyo nayo ambayo inafananishwa na usaliti alioutenda Yuda kwa Yesu," alisema Askofu Dallu.

Pia alieleza kusikitishwa kuona kwamba katika muda mfupi bidhaa mbalimbali zimepanda na kusababisha hali ngumu ya maisha kwa wananchi, akitolea mfano bidhaa ya mchicha unaolimwa hapa hapa nchini kupanda bei kwa kisingizio cha vita vya Ukraine na Russia.

Alisema serikali inapaswa kutazama kwa mapana tatizo la kupanda bidhaa holela hali ambayo inawaumiza wananchi.

# Wawashtaki wauguzi na madaktari kwa RC

**Na Ibrahim Yassin,** TUNDUMA

WANANCHI wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Momba mkoani Songwe, wamewashtaki wauguzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, kwa madai kwamba wamekuwa wakichati au kuchezea simu badala ya kuwahudumia wagonjwa.

Wamesema wauguzi hao wamekuwa wakitenda vitendo hivyo hata kukiwa na mgonjwa mahututi.

Walieleza malalamiko hayo juzi wakati wa mkutano wa hadhara wa kumaliza migogoro ya ardhi ulioitishwa na mkuu huyo wa mkoa katika kata ya Mpemba huku wakielezea kero mbalimbali zinazowakabili na kuibua madai hayo dhidi ya wauguzi.

Mkazi wa Tunduma, Sarafina Mathias, alisema imekuwa kawaida kwa madaktari na wauguzi kuchati au kuchezea simu zao kwa kucheza michezo wakati wagonjwa wakihitaji huduma za haraka.

Alisema yeye ni miongoni mwa waathirika wa vitendo hivyo na kwamba aliwahi kufika katika Kituo cha Afya Tunduma na kutohudumiwa kwa haraka.

Samwel Mtafya, Mkazi wa Mpemba, alisema siku moja alimpeleka baba yake kupata matibabu katika Kituo cha Afya Tunduma lakini alipofika alishangaa kuona muuguzi akichati na simu huku mzee wake akiwa hoi akihitaji kupatiwa matibabu na kwamba alipoenda kwa daktari akakuta yupo bize anachezea simu.

Kutokana na kero hizo, Mgumba alimwinua Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Dk. Stephen Kalobo, kujibu tuhuma hizo kabla ya kutoa maelekezo.

Dk. Kalobo alisema: "Ni kweli malalamiko hayo yapo lakini yanatokana na uelewa mdogo kwa baadhi ya wananchi ambao wakiona wauguzi wako bize na kompyuta wanadhani wanachati bila kujua kuwa sasa hivi hawatumii kuandika taarifa kwa karatasi.

Alisema awali walikuwa wakiandika maelezo ya wagonjwa kwa kutumia karatasi lakini kwa sasa mambo yote yanafanyika kidigitali, hivyo wauguzi wanapoingiza taarifa zao kwenye kompyuta wao wanadhani kuwa wanachati na kwamba ipo haja elimu zaidi ipite ili wananchi wajue.

Dk. Kalobo alisema Halmashauri ya Mji wa Tunduma imepata dawa asilimia 92, hivyo vituo vilivyopo vina ngazi mbalimbali za kutoa dawa na mgonjwa anapoambiwa dawa anazotakiwa apatiwe hazipo aende ngazi nyingine ama hospitali fulani anaona kama ni kero wakati ndiyo kawaida ilivyo.

Akizungumza katika mkutano huo, Mgumba alitoa siku 30 kuhakikisha Hospitali ya Wilaya iliyo katika asilimia 80 za ujenzi ianze kufanya kazi ya kuhudumia wananchi wakati ujenzi ukiendelea.

## Mambo ya kutisha yaibuliwa magereza

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini upungufu wa fedha kwa ajili ya miundombinu ya rumande na magereza unaosababisha msongamano katika magereza nchini.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Jumanne ya wiki hii, CAG anasema kuwa kwenye magereza aliyoyatembelea, amebaini kuwa na msongamano kati ya asilimia moja na 194 zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa.

Anasema kiwango kikubwa cha msongamano kilibainika mkoani Dar es Salaam katika Gereza la Keko, ambalo lilikuwa na msongamano wa zaidi ya asilimia 194.

CAG anafafanua kuwa kiwango kilichoidhinishwa katika Gereza la Keko ni wafungwa na mahabusu 340, lakini wakati wa ukaguzi wake alibaini kuwapo wafungwa na mahabusu 999, sawa na kuzidi kwa asilimia 194.

Anabainisha kuwa mkoani Lindi kwenye Gereza la Kingurungundwa, alikuta wafungwa na mahabusu 88 ilhali kiwango kilichoidhinishwa ni 39, hivyo kuzidi kwa asilimia 126.

Pia kwenye Gereza la Kiomboi mkoani Singida, CAG anasema alikuta wafungwa na mahabusu 132 ilhali uwezo wa gereza ni wafungwa na mahabusu 58, hivyo kuzidi kwa asilimia 128.

Mkoani Mwanza kwenye Gereza la Butimba, CAG anasema alikuta wafungwa 1,247 wakati kiwango kilichoidhinishwa ni 934, hivyo kuzidi kwa asilimia 34.

Kwenye Gereza la Segerea jijini Dar es Salaam, CAG anabainisha kuwa alikuta wafungwa na mahabusu 1,552 ilhali kiwango kilichoidhinishwa ni 1,036, hivyo kuzidi kwa asilimia 50.

"Ukaguzi ulihakiki majengo ya makazi ya magereza na kubaini kuwa mengi ni chakavu na yanahitaji ukarabati mkubwa. Hali mbaya zaidi ilibainika katika magereza ya kilimo ambapo wafungwa walikuwa wakilala katika vyumba zilivyojengwa kwa mabati.

"Hali hii ilibainika katika Magereza ya Kilimo ya Ushora na Kingurungundwa. Nyumba nyingi za wafanyakazi wa magereza zilizotembelewa zilikuwa katika hali mbaya kwa sababu ya ukosefu wa matengenezo na ukarabati.

"Nyumba za watumishi wa magereza zilikosa maji safi na ya kutosha. Mifumo ya majitaka ilikuwa chakavu na mingi ilikuwa ikivuja. Hali hii ilibainika katika magereza sita ambayo ni magereza makuu ya Keko na Butimba; magereza ya Wilaya za Kilwa, Manyoni na Ukerewe; na magereza ya kilimo ya Kingurungundwa na Kwa Mngumi," anasema.

CAG anabainisha kuwa Jeshi la Magereza halikuwa na mipango ya matengenezo ili kusaidia shughuli zake za ukarabati wa majengo na hakukuwa na bajeti iliyotengwa kwa madhumuni ya ukarabati na matengenezo.

Anasema kuwa kutokana na ukarabati na matengenezo hayo ya miundombinu ya magereza kukosa bajeti, shughuli hizo ziliachwa kwa magereza husika ambapo ukarabati ulifanyika kwa kutumia vyanzo vya fedha vya ndani vya magereza husika.

"Kutokana na ufinyu wa fedha, ukaguzi ulibaini kuwa kwa magereza yote 15 yaliyotembelewa, Sh. milioni 38 zilipelekwa kwa magereza husika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari isipokuwa Wilaya ya Ukerewe iliyopokea Sh. milioni 76 kutokana na hali ya nyumba za maofisa wa magereza kuwa mbaya zaidi.

"Imeelezwa kuwa fedha zilizotolewa zilitoka katika vyanzo mbalimbali kama vile faida iliyotokana na miradi ya uwekezaji inayotekelezwa na Jeshi la Magereza nchi nzima," CAG anabainisha.



Abiria wakishuka kutoka kwenye gari aina ya Toyota Landcruiser lenye namba za usajili T 728 AHK, baada ya kumshinda dereva na kutumbukia kwenye mtaro wa maji ya mvua katika eneo la Uhasibu, Barabara ya Kilwa, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mkandarasi apewa zabuni, aiuza kisiri kisha kujipatia mabilioni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini mkandarasi aliyepewa kazi na Mamlaka ya Bandari (TPA) kumpa kazi hiyo mkandarasi mwingine bila kutoa taarifa kwa mamlaka.

Vilevile, amebaini kufanyika malipo zaidi ya gharama halisi za mradi huo kwa Sh. bilioni 64.30, akipendekeza serikali ichukue hatua stahiki dhidi ya wahusika.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumanne ya wiki hii, CAG Charles Kichere anasema TPA iliingia mkataba na mkandarasi mkuu wa Sh. bilioni 172.36 Agosti 3, 2019 wa muda wa mwaka mmoja hadi kufikia mwezi Agosti 2020 kwa ajili ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli katika Bandari ya Tanga.

Anabainisha kuwa mkataba huo pia ulijumuisha kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kununua vifaa kwa ajili ya shughuli za bandari.

CAG anasema kuwa kulingana na mkataba, gharama ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli katika Bandari ya Tanga ilikuwa ni Sh. bilioni 104.92 (asilimia 60 ya bei yote ya mkataba).

Hata hivyo, CAG anabainisha kuwa mnamo Agosti Mosi 2019, mkandarasi mkuu iliingia makubaliano na mkandarasi mbia kwa ajili ya kazi ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli kwa bei ya mkataba dola za Marekani milioni 18.15, sawa na Sh. bilioni 40.46 kwa kipindi cha miezi 11 bila kutoa taarifa kwa TPA.

"Mkandarasi mkuu pia aliingia mkataba na mkandarasi mbia hata kabla ya kutia saini mkataba wake na TPA. Kuingia mkataba bila kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Bandari ni kinyume cha kifungu kidogo cha 4.4 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kati ya TPA na mkandarasi mkuu ambacho kinaizuia mkandarasi mkuu kutoa sehemu ya kazi kwa mkandarasi mwingine.

"Na ikiwa kuna uhitaji wa kutoa kazi kwa kampuni nyingine kutekeleza kazi zilizoko kwenye mkataba, mkandarasi mkuu anapaswa kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Bandari siku 28 kabla ya kutoa kazi hiyo.

"Vilevile, nilibaini jumla ya malipo yaliyolipwa kwa kazi ya kuongeza kina cha lango na sehemu ya kugeuzia meli yalikuwa dola za Marekani milioni 18.22, sawa na Sh. bilioni 40.62.Kiasi hiki pia kinajumuisha malipo ya dola za Marekani 73,824, sawa na Sh. milioni 164.55 kwa huduma za wakala wa meli kwa mkandarasi mbia.

"Ulinganifu wa kiasi kilichotozwa na mkandarasi mkuu Sh. bilioni 104.92 na kiasi alicholipwa na mkandarasi mbia Sh. bilioni 40.62 inaonyesha kiasi kilichotozwa na mkandarasi mkuu kimezidi kiasi halisi kilichotumika kufanya malipo ya kazi hiyo kwa Sh. bilioni 64.3," anasema.

CAG anapendekeza TPA na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuchukua hatua kutokana na udanganyifu wa bei uliofanywa na mkandarasi mkuu; pia kuchukua hatua kwa maofisa waliopaswa kufanya utafiti wa gharama ili kujua makisio halisi ya bei kabla ya kuingia mkataba na mkandarasi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya
Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI
Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA
Usimamizi wa mirathi Na 21/2022
KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU ANYELWISYE DUSTAN WA NKUHUNGU
KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA CATHERINE KILUNGU


**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 Mwezi 04 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe **11 Mwezi 02 Mwaka 2022**

..............................................
**HAKIMU**


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA U J E N Z I , UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470DODOMA,
21.03.2022

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya **tarehe 19.04.2022 hadi 05.05.2022** kampuni ya Spedag Interfreight itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Holili kuelekea Moshi, gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW052Z / ZG3212**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

   **Urefu - Mita 28.4 Upana - Mita 5.0 Kimo - Mita 5.6**

3. Njia itakayotumika: Holili hadi Moshi kupitia Soweto, gari litasafiri muda wa mchana tu ( **Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

# Walia kupanda nauli za bajaji

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

WAKAZI wa Manispaa ya Songea wamelalamikia kupanda kwa nauli za bajaji kutoka Sh. 500 hadi Sh. 700, huku wakidai hali hiyo inawaumiza kimaisha.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wananchi hao walisema wameshtushwa na kupanda kwa bei ya usafiri wa bajaji katika manispaa hiyo.

Mwanaidi Khamis, mmoja wa wakazi hao, alisema kupanda kwa nauli kumewaongezea gharama za maisha kwa sababu wakazi wengi wa Songea maisha yao ni duni.

Naye Bakari Hamza alisema kitendo cha kupandisha nauli ya bajaji kimesababisha wananchi wengi kutembea kwa miguu kwenda katika shughuli zao na kwamba kiwango kilichoongezwa ni kikubwa.

"Serikali tunaiomba iingilie kati kwa sababu tunaoumia ni sisi wananchi. Wao ukiwauliza kwa nini wamepandisha nauli wanasema gharama za mafuta zimepanda," alisema Hamza.

Wananchi hao wameiomba serikali serikali kudhibiti kupanda kwa bei hiyo pamoja na wafanyabishara kupandisha bei ya bidhaa pasipo kufuata utaratibu.

Akizungumza na Nipashe, Kiongozi wa Chama cha Waendesha Bajaji Manispaa ya Songea, Salvatory Mangasila, ambaye alithibitisha kupanda kwa nauli za bajaji na kuwaomba wakazi wa Songea kuwaunga mkono kuendelea kutumia usafiri huo na kwamba sababu ya kupanda kwa nauli hizo ni kutokana na kupanda kwa mafuta.

"Sisi hakuna namna, ni lazima tupandishe nauli kwa sababu bei ya mafuta nayo imepanda, tusipopandisha tunapata hasara, hivyo ni lazima tupandishe ili tupate pesa pamoja na hesabu ya tajiri," alisema kiongozi huyo.

Nipashe liliwatafuta viongozi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) mkoani Ruvuma ili watoe ufafanuzi wa hali hiyo lakini hawakupatikana kutokana na kuwa katika mapumziko ya mwishoni mwa wiki na sikukuu ya Pasaka.

# Tanzania kunufaika ufadhili madini EU

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imechaguliwa kuwa moja ya nchi nne wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Afrika, Caribbean na Pacific zitakazonufaika na programu ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya (EU), kupata Euro milioni 11.1 (Sh.bilioni 30) kwenye sekta ya madini.

Taarifa iliyotolewa jana na Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ilisema programu hiyo inalenga kuboresha mazingira ya uchimbaji madini, kuwajengea uwezo wachimbaji wadogo hususani vijana na wanawake kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2022 - 2024.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa uamuzi huo umetangazwa na Sekretarieti ya OACPS, ambayo makao makuu yake yako Brussels, Ubelgiji.

Mbali na Tanzania, nchi zingine tatu za Jumuiya ya Afrika, Caribean na Pacific zilizofanikiwa kuchaguliwa kwenye programu hiyo ya awamu ya pili ni Burkinafaso, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Suriname.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, utekelezaji wa programu hiyo utachochea sekta ya madini katika nchi za OACPS kutoa mchango stahiki katika kuongeza mnyororo wa thamani ya madini, uzalishaji wa nafasi za ajira na ukuaji wa uchumi.

"Upatikanaji wa nchi za kunufaika na awamu ya pili ya programu hii uliyoanza mchakato wake Agosti mwaka jana, ulikuwa na ushindani mkubwa kutokana na idadi kubwa ya nchi zilizojitokeza kuomba zijumuishwe," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

"Jumuiya ya OACPS ina nchi 79, hivyo kuchaguliwa kwa Tanzania kunufaika na programu hii ni matokeo ya kuendelea kuimarika kwa ushawishi wa Tanzania ndani ya Jumuiya ya OACPS na kazi nzuri inayofanywa na Serikali katika kuimarisha ushirikiano na jumuiya hiyo kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na ubalozi wa Tanzania ulioko Brussels, Ubelgiji"," taarifa hiyo iliongeza.

Utekelezwaji wa programu hiyo utafanywa kwa ushirikiano kati ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Wizara ya Madini chini ya ufadhili wa EU.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar (Mazingira), Hamza Hassan Juma (kushoto), akikabidhi Tuzo kwa Kassim Ayubu, baada ya kuibuka mshindi wa kwanza aliyehifadhi judhuu 30 katika mashindano ya saba ya kuhifadhi Qur'an Tukufu, yaliyoandaliwa na Taasisi ya Asw Haabul Kahfi Islamic Centre na kudhaminiwa na Benki ya CRDB, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mlezi wa taasisi hiyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Seleman Jafo (wa pili kushoto nyuma), Mwenyekiti wa Jumuiya ya kuifadhisha Qur'an, Sheikh Othuman Kapolo (kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Al- Barakah wa benki hiyo, Rashid Rashid. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Utafiti jotoridi kuzalisha umeme waanza

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) imesema itaanza kuchoronga visima vifupi vya utafiti katika Mradi wa Jotoardhi Songwe, vitakavyosaidia kuzalisha umeme wa megawati tano ifikapo mwaka 2023.

Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, aliyasema hayo juzi alipofanya ziara katika eneo utakapotekelezwa mradi huo katika Kijiji cha Nanyala wilayani Mbozi, Mkoa wa Songwe huku akibainisha kuwa mchakato wa kuchoronga utaanza mwezi ujao.

Lengo la ziara hiyo lilikuwa kujionea hali ya eneo hilo, hatua zilizofikiwa hadi sasa za uendelezaji wa rasilimali hiyo ya jotoardhi pamoja na hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha mradi huo unatekelezwa ili kuweza kupata umeme kutokana na nishati hiyo.

Alisema serikali imejikita katika kuendeleza nishati jadidifu ambazo ni endelevu, salama na rafiki wa mazingira kama vile jotordhi ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na uhakika wa uzalishaji umeme nchini.

Mramba alisema nishati nyingine kama gesi asilia ambayo inazalisha umeme kwa kiasi kikubwa kwa sasa nchini huwa inaisha tofauti na nishati jadidifu kama ya jotoardhi.

Alisema wakati TGDC ikiwa kwenye mpango wa kuanza kuchoronga visima vya majaribio na vya kuzalisha mvuke, wanapaswa kuwa na hatimiliki ya eneo hilo.

Kaimu Meneja Mkuu wa TGDC, Mhandisi Mathew Mwangomba, alimweleza Mhandisi Mramba kuwa mradi huo ulianza kutekelezwa mwaka 2018 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2023/24.

Alisema pamoja na kujipanga na kuanza kazi ya kuchoronga visima, TGDC inaendelea na utekelezaji wa miradi ya matumizi mengine katika eneo la mradi ikiwamo kuongeza thamani ya mazao ya mifugo.

Aliongeza kuwa, miradi mingine inayoendelea kutekelezwa kutokana na uwapo wa nishati ya jotoardhi ni pamoja na uendelezaji wa kilimo, kwamba kutajengwa nyumba kitalu kuongeza thamani ya mazao ya kilimo kama kukausha mazao kwa kutumia joto na kuboresha vivutio vya utalii vinavyopatikana katika maeneo hilo.

## HABARI KITAIFA

# Barabara yafungwa kisa ujenzi daraja

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

BARABARA kutoka Matarawe hadi Mjimwema katika Manispaa ya Songea, imefungwa baada ya Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) wilayani Songea kuanza ukarabati baada ya daraja lililokuwapo awali kubomolewa na mvua.

Akizungumza na Nipashe, Meya wa Manispaa ya Songea, Michael Mbano, alisema barabara hiyo imefungwa kuanzia juzi ili kupisha ujenzi wa daraja hilo ambalo linatarajiwa kukamilika baada ya miezi miwili kuanzia hivi sasa.

Mbano ambaye pia ni Diwani wa Msamala, alisema jitihada za serikali kupitia TARURA zimefanywa kwa kuhakikisha daraja hilo linajengwa haraka ili wananchi wanaokwenda kupata huduma kwenye Kituo cha Afya Mjimwema wavuke.

Diwani wa Mjimwema, Sylvester Mhagama, aliipongeza serikali kwa kuchukua hatua za haraka za kukarabati daraja hilo linalounganisha barabara ya Matarawe kwenda Mjimwema ambalo lilibomolewa na mvua Aprili 10, mwaka huu.

Alisema kubomoka kwa daraja hilo kumesababisha wakazi wa maeneo ya Misufini, Matarawe, Mabatini na Mjimwema kupata adha wakati wanapokwenda kupata matibabu kwenye Kituo cha Afya cha Mjimwema pamoja na Soko la Manzese.

Diwani wa Matarawe, Judith Mbogoro, alisema wakazi wa kata hiyo na maeneo mengine wamekuwa wakitegemea kupata matibabu kwenye Kituo cha Afya cha Mjimwema, lakini kuharibika kwa daraja hilo kumesababisha kutumia muda mrefu kufika kwenye kituo hicho kutokana na kuharibika kwa daraja hilo.

Wakizungumza na Nipashe, mmoja wa wakazi wa Mjimwema, John Komba, alisema kubomoka kwa daraja hilo kumeleta usumbufu kwa wakazi wanaoishi maeneo ya Mwenge Mshindo, Luwawasi na Mjimwema kwani wanapohitaji kwenda Soko Kuu la Mjini na Manzese au kwenda kupata huduma kwenye ofisi za serikali ambazo ziko Songea Mjini wanachukua muda mrefu kufika.

Aliiomba serikali iharakishe kulitengeneza daraja hilo ambalo ni kiungo kikubwa kwa wakazi wa Luwawasi, Mwengemshindo, Mjimwema na Matarawe.

# Wizara yatoa kibali cha ajira 1,650 afya

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imetoa kibali cha ajira za watumishi 1,650 wa kada mbalimbali za afya, ambao wataajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi vilivyoko chini ya Wizara ya Afya.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, ilisema kibali hicho kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kitatoa fursa kwa wataalamu wa kada mbalimbali katika vituo vya kutoa huduma, chini ya uendeshaji wa Wizara ya Afya.

Prof. Makubi alisema kada ambazo zitanufaika na nafasi hizo na idadi kwenye mabano ni madaktari bingwa (250), madaktari (2,150), wafamasia (15), maofisa maabara (62), wateknolojia-dawa, maabara, mionzi na macho (155), maofisa uuguzi (140), maofisa uuguzi wasaidizi (467), wauguzi (140), wakemia wawili na madaktari wa afya kinywa na meno (15).

Wengine ni matabibu meno (19), watoa tiba kwa vitendo (15), wazoeza viungo kwa vitendo (31), maofisa wazoeza viungo (33), maofisa afya mazingira (40), wasaidizi wa afya (134), wahandisi vifaa tiba (17), wateknolojia vifaa tiba (40), watunza kumbukumbu wa afya (10) na madereva wanne.

"Ajira hizo zinategemewa kwenda kupunguza uhaba wa watumishi kutokana na serikali kujenga hospitali mpya pamoja na kuendeleza miundombinu ya utoaji wa huduma za afya," alisema.

Aidha, alisema waombaji watakaochaguliwa watapangiwa kazi kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa wa wataalamu wa kada za afya na hakutakuwa na kubadilisha kituo cha kazi ndani ya miaka mitatu.

Profesa Makubi aliyataja maeneo hayo kuwa ni hospitali za rufani za mikoa ya Kigoma, Katavi, Sumbawanga, Songwe, Njombe, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Simiyu, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Manyara na Mara. Pia alisema katika kundi hilo, zimo Hospitali za Kanda za Chato na Mtwara,

Alisema waombaji wawe tayari kupangiwa katika maeneo husika, huku akisisitiza kuwa ambao hawatakuwa tayari kwenda kwenye maeneo tajwa wanashauriwa kutotuma maombi.

Prof. Makubi alisema waombaji walioko masomoni hawaruhusiwi kuomba nafasi hizo za ajira.

Pia alisema mwombaji atapaswa kuchagua maeneo matatu ambayo angependa kupangiwa kazi endapo atachaguliwa, mwenye nia ya kwenda kufundisha katika vyuo vya afya aainishe wakati wa kutuma maombi kwenye mfumo pamoja na barua ya maombi.

"Muda wa kutuma maombi hayo ni ndani ya wiki mbili tangu tangazo litoke ambao ni jana (juzi) na maombi yote yawasilishwe kupitia mfumo wa ajira wa Wizara ya Afya unaopatikana kupitia tovuti ya ajira.moh.go.tz. atakayeomba kupitia tovuti hiyo asiombe kwa nafasi hiyo hiyo kwa upande wa OR-TAMISEMI."



Mafundi wa Shirika la Ugavi la Umeme Tanzania (TANESCO), wakikarabati nyaya za umeme katika eneo la Ilala, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uhaba wa mafuta mpakani wazua balaa

**Na Samson Chacha,** TARIME

WANANCHI katika mji wa Isabania, mpakani mwa Tanzania na Kenya, wanakabiliwa na uhaba wa mafuta, hali inayowalazimu kuvuka mpaka kuingia Tanzania kununua na kwenda kuyauza kwa bei ya juu nchini mwao.

Wafanyabiashara hao wanavuka mpaka wakiwa wamebeba madumu, wengine wakiwa na pikipiki kuingia na kununua mafuta katika mji wa Sirari.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wakazi wa mji wa Isebania, Kenya na Sirari, Tanzania walisema mji huo umekumbwa na uhaba wa mafuta ya magari kwa takribani wiki moja.

Marwa Wambura, mmoja wa wakazi kutoka upande wa Kenya, alisema inawalazimu kuingia Tanzania katika kituo cha Sirari kununua mafuta yanayouzwa lita moja kwa Sh. 3,050, kwenda kuyauza Kenya kwa Sh. 170 (sawa na Sh. 3,500 za Tanzania).

"Tukishanunua tunayahifadhi kwenye madumu na kuyalaza ndani ya nyumba. Ni hatari kwa usalama wetu pindi majanga ya moto yanapotokea lakini inatulazimu kufanya hivyo," alisema Marwa. Mkazi mwingine, Mangera Chacha, alisema: "Mji wa Sirari kuna magari na pikipiki kwa wingi na kuna vituo vidogo vya kuuza mafuta viwili ambapo mara nyingi kituo kimoja ndicho hufanya kazi hali inayochangia kuwapo na mlundikano na msururu wa magari na pikipiki.

"Huku kumekuwa na urasimu na ukiritimba kwa baadhi ya wafanyabiashara kuwapiga vita wenzao wanaotaka kuwekeza katika Mji wa Sirari hususani katika vituo vya mafuta. Tunaomba serikali itupie macho".

Alisema urasimu huo unawakwamisha baadhi ya wafanyabiashara wazalendo wanaotaka kuwekeza katika mji huo.

Pia alisema hali hiyo inakwamisha juhudi za maendeleo kwa wananchi na kwa taifa kwa kukosa mapato ambayo yangepatikana kutokana na kuwapo kwa wingi kwa vituo vya mafuta.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Sikukuu ya Pasaka ilete mabadiliko katika jamii

**LEO** ni Sikukuu ya Pasaka. Ni siku ambayo Wakristo duniani kote wanaadhimisha kufufuka kwa Mwokozi wao, Yesu Kristo baada ya kuteswa hadi kufa yapata miaka 2,000 iliyopita.

Pasaka pia ni hitimisho la mfungo wa Kwaresma wa siku 40 ambao baadhi ya waumini hufunga tangu kuanza kwa siku maalumu ya Jumatano ya Majivu.

Ni sikukuu ambayo huwakusanya waumini katika ibada zinazofanyika katika makanisa na madhehebu mbalimbali zikifuatiwa na ibada za siku ya pili ambazo zitafanyika kesho kwenye mikusanyiko tofauti zikiwamo ibada za umoja wa makanisa kwa hapa nchini kama zilivyotangazwa.

Wakati wa ibada hizo, kwa Tanzania, viongozi wa dini hasa maaskofu, mapadri na wachungaji, hutoa ujumbe mzito ukiwamo wa kumcha Mungu pamoja na masuala yanayohusu jamii katika wakati husika kama ilivyokuwa juzi wakati wa ibada za Ijumaa Kuu.

Licha ya kusherehekewa kwa ibada, sikukuu hii huambatana na watu kufanya tafrija mbalimbali majumbani ikiwamo kuandaa vyakula na vinywaji pamoja na kuwakaribisha ndugu, jamaa na marafiki.

Pia kuna watu wachache ambao husafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa ajili ya kuadhimisha siku hii.

Sikukuu hii pia husherehekewa kwa watu kukusanyika kwenye majumba ya starehe kwa ajili ya kunywa na kula huku kukiwa na burudani za muziki na shughuli mbalimbali kwenye maeneo ya starehe kama vile fukwe za bahari.

Kwa ujumla, ni sikukuu ambayo huwa na shamrashamra mbalimbali za watu wa rika tofauti.

Kutokana na unyeti wa sikukuu yenyewe na marejeo ya mambo yaliyotokea ikiwamo watoto kupotea na uvunjifu wa amani katika baadhi ya maeneo, Jeshi la Polisi kupitia makamanda wa mikoa na kanda, limeshatoa tahadhari dhidi ya watu watakaosababisha uvunjifu wa amani.

Pia wazazi na walezi wametakiwa kutowapeleka watoto kwenye mikusanyiko ambayo inaweza kusababisha athari za kisaikolojia na makuzi kwao.

Pamoja na dhana kujengeka kwamba Pasaka ni sikukuu yenye shamrashamra mbalimbali, ni vyema Wakristo ambao wanaamini kwamba Yesu Kristo amefufuka kwa ajili ya ukombozi wao na kuwatoa katika vifungo mbalimbali vya kimaisha, wanapaswa kutafakari na kubadilika kifikra na kimaisha.

Sikukuu hii iwafanye wabadilike na kutenda matendo mema kama ilivyokuwa kwa baadhi waliojizuia kufanya mambo kadhaa wakati wa Kwaresma.

Lakini pia Watanzania, bila kujali imani zao, wanapaswa kuzingatia mawaidha na mafundisho watakayopewa katika ibada za Pasaka pamoja na yale yaliyozungumzwa na viongozi wao wakati wa ibada za Ijumaa Kuu. Kwa maneno mengine, wanapaswa kutambua kwamba Pasaka ni sehemu ya kujitafakari juu ya maisha ya duniani na ahera, hivyo kuishi vyema kwa kufuata mafundishio na maisha ya Yesu Kristo alipokuwa duniani.

Kwa mantiki hiyo, Pasaka ya mwaka huu iwe na mabadiliko kwa jamii katika kutenda haki na kuwajali watu wenye mahitaji.

Kwa wale waliopewa dhamana ya uongozi katika ngazi mbalimbali, wawe kielelezo na ushuhuda mwema katika kutenda haki.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hujuma za miundombinu ya elimu zisipewe nafasi

**KWA** mara ya kwanza, wanafunzi wote waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza mwaka huu, katika shule mbalimbali nchini, wameanza masomo kwa pamoja tofauti na miaka iliyopita.

Miaka ya nyuma, wanafunzi walikuwa wakianza masomo kwa awamu mbili hadi tatu na sababu kubwa ilikuwa uhaba wa vyumba vya madarasa lakini safari hii, serikali imefanya kila jitihada ya kumaliza tatizo hilo.

Shule nyingi za sekondari, zimekuwa na madarasa ya kutosha ambayo yamejengwa kwa fedha za Mpango wa Maendeleo wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19, hivyo kumaliza kero hiyo nchini.

Lakini wakati serikali ikiwa imejitahidi kuhakikisha inamaliza kero, inaonekana wako baadhi ya watu wasiopenda maendeleo hayo kwa kufanya hujuma kwenye miundombinu ya elimu.

Miongoni mwa hujuma hizo ni zile zilizotangazwa na vyombo habari kuhusu uvunjaji vya vioo vya madarasa ya Shule ya Sekondari Kibedya, Gairo mkoani Morogoro na kusababisha mkuu wa shule hiyo kusimamishwa kazi. Amesimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi baada ya madarasa 12 yaliyojengwa kwa fedha za maendeleo na zile za mapambano dhidi ya UVIKO-19, maarufu kama madarasa ya Mama Samia, kuhujumiwa.

Inaelezwa kuwa Gairo ilipokea Sh. bilioni 1.1 kutoka kwenye mpango huo ili kuboresha miundombinu ya elimu ambayo sasa imehujumiwa hali ambayo inaweza kurudisha nyuma maendeleo ya sekta hiyo.

Ninadhani umefika wakati sasa wananchi kutambua kuwa shule za umma ni mali yao, wanapaswa kulinda miundombinu yake kwa manufaa ya watoto wao, badala ya kujiweka kando na kudhani hawahusiki.

Ili kufanikisha ulinzi wa miundombinu ya shule, ni vyema wakaweka walinzi wa uhakika ambao watafanya kazi hiyo bila kurubuniwa kwa namna yoyote kwa ajili ya kuhakikisha wanatimiza wajibu wao kikamilifu.

Lakini pia ni vyema kila mwananchi akatambua kuwa ni mlinzi wa mali ya umma kwa maana kwamba anaposikia au kuona mikakati ya hujuma inafanyika, ni muhimu akatoa taarifa kwa vyombo husika ili hatua za kudhibiti zichukuliwe.

Kwa mfano, inaelezwa kuwa mlinzi wa shule hiyo alihojiwa na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya, na kukiri kuwa siku ya tukio hakuwapo eneo lake la kazi, na kwamba siku ya tukio hakukuwa na umeme.

Kisa ni kwamba, Luku iliisha muda mrefu bila kununuliwa umeme mwingine. Ninaamini kama wananchi wangekuwa wanafuatilia kwa karibu, wangegundua hilo na kuchukua hatua ikiwamo kutoa taarifa.

Si vibaya kama wangeukumbusha uongozi wa shule kununua umeme, kwani inaelezwa kuwa pamoja na Luku kuisha, uongozi haukuchukua hatua zozote, lakini ingekuwa vyema kama nao wangetimiza wajibu wao.

Imeripotiwa kuwa katika shule hiyo, ni vioo vya madarasa 12 yaliyogharimu zaidi ya Sh. milioni 120, na sasa inalazimika kipatikane kiasi kingine kama hicho kurudishia vioo vingine kwa madarasa hayo.

Fedha ambazo zitatumika kuweka vioo vipya, zingepelekwa kuboresha huduma nyingine katika jamii, lakini sasa kutokana na hujuma hiyo, inalazimika viwekwe vingine kwenye madarasa hayo. Serikali ilipanga kujenga madarasa 12,000 katika shule za sekondari kwa gharama ya Sh. bilioni 240 katika halmashauri mbalimbali nchini kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka huu.

Ujenzi wa idadi hiyo ulitokana na mahitaji kulingana na idadi ya wanafunzi waliotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, huku matokeo ya ufaulu kitaifa yakiwa yanatofautiana kati ya halmashauri moja na nyingine. Serikali pia ilitoa maelekezo kwa watendaji kuhakikisha fedha hizo zinatumika kama ilivyokusudiwa, lakini pia ujenzi ulingane na thamani ya fedha zilizotumika na siyo kuchakachua.

Inawezekana watendaji kwa sehemu yao walijitahidi kufuata maelekezo ya serikali, lakini sasa zimeanza kujitokeza hujuma hizo za miundombinu ya elimu, hali ambayo inaweza kuiingiza serikali kwenye gharama nyingine. Ninadhani tukio la Gairo, liwe mwanzo kwa wananchi ambao wamekuwa hawatambui kuwa shule za umma ni mali yao, basi washtuke na kufuatilia hatua kwa hatua kwa ajili ya kudhibiti matukio ya aina hiyo.

Wananchi ni wadau wakubwa wa elimu, hivyo ingekuwa ni vyema wakahakikisha miundombinu ya elimu haihujumiwi kwa namna yoyote ikiwamo kama ilivyotokea huko Gairo.

SAFU

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Hongera sana Rais Samia lakini ingenoga iwapo ungalifanya hivi



Na Pascal Mayalla

**Naunga mkono uzinduzi wa Royal Tour kufanyikia Marekani. Ni mahali sahihi Kwa sababu huko ndiko kwenye 'catchment areas' za watalii wenye fedha. Pia kwa mawazo yangu, kwa vile lengo, pamoja na mambo mengine, ni kuutangaza utalii wetu hususan vivutio vilivyopo ili kuhamasisha watalii wengi zaidi kuitembelea Tanzania, hakuna kitu kinachoongoza kwa kutangaza utalii kama usafiri wa ndege wa moja kwa moja.**

KWA vile leo ni Jumapili ya Sikukuu ya Pasaka, nianze kwa kuwatakia heri za Pasaka kwenu nyote na kwa wenye majina ya Paskali, Paschal, Pascal, Pasco, Pascalia na Easter ambao walizaliwa siku ya Pasaka. Nawatakia heri ya kuzaliwa.

Makala ya leo ikiwa ni ya swali la kufikirika, kwa njia ya "thinking aloud", yaani unawaza kwa sauti, ni mwendelezo wa makala iliyotoka siku za nyuma ikimpongeza Rais Samia kwenda Marekani kuhutubia kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa.

Katika makala hiyo, niliuliza kwa nini Rais wetu atumie ndege za watu wengine wakati sasa na sisi tunazo ndege zetu?. Nikashauri siku akienda kuzindua filamu yake ya Royal Tour, aende na ndege yetu na ikibidi Watanzania wenye uwezo tumsindikize.

Hivi ninavyozungumza, tayari Rais Samia yuko Marekani kwa ajili ya uzinduzi wa filamu yake ya Royal Tour, utakaofanyika kesho lakini kama ilivyokuwa awali, amekwenda tena na ndege za watu.

Swali ni je, uzinduzi wa filamu ya Royal Tour, unaofanyikia Marekani, ungekuwa na maslahi makubwa zaidi kwa taifa kama Rais Samia angetua huko kwa dege letu la Dreamliner, huku Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) likizindua safari za moja kwa moja za Tanzania na Marekani au kuendelea kwenda kwa ndege za watu, kuzindua, kushangilia, halafu hao watalii wa Marekani tunaowahamasisha kuja Tanzania, wakitaka kuja, waje kwa ndege za watu, huku midege yetu tumeipaki?

Japo mimi si mtaalamu wa usafiri wa anga, kusafiri nchi mbalimbali na katika masafa mbalimbali, kumenipa upeo mkubwa na wa kutosha kuwaza kwa sauti na kuuliza swali hili.

Kwanza, nitoe pongezi kinara au mhusika mkuu wa 'movie' hiyo. Mtu kuwa 'sterling' wa 'movie' yoyote kiukweli si mchezo bali ni kipaji. Kwa jinsi nilivyoziona zile 'pati gazeti' za filamu hii, "trailers", kiukweli kabisa angekuwa ni Nyerere, asingeweza!, Mwinyi, asingeweza!, Mkapa ndio kabisa!, na JPM asingekubali hata kuruhusu! Mtu mwingine ambaye angalau angeweza kuwa 'starling' wa 'movie' kama hii ni Jakaya Kikwete, maarufu kama JK, tena angepatia zaidi kwa sababu ni "hechibii" kuwakaribia Steven Kanumba, Will Smith, Denzel Washington or Sidney Pointer.

Naunga mkono uzinduzi wa Royal Tour kufanyikia Marekani. Ni mahali sahihi Kwa sababu huko ndiko kwenye 'catchment areas' za watalii wenye fedha. Pia kwa mawazo yangu, kwa vile lengo, pamoja na mambo mengine, ni kuutangaza utalii wetu hususan vivutio vilivyopo ili kuhamasisha watalii wengi zaidi kuitembelea Tanzania, hakuna kitu kinachoongoza kwa kutangaza utalii kama usafiri wa ndege wa moja kwa moja.

Hakuna kitu kinachoitangaza nchi kimataifa kama kupeperusha bendera ya nchi moja kwenye nchi nyingine. Hakuna kitu kinaipeperusha vizuri bendera ya nchi kimataifa kama ndege inayotambulisha nchi, yaani ndege za mashirika ya kitaifa kutua viwanja vya nchi zingine.

Rais Samia hasafiri safari za mbali kwa ndege zetu ili kukwepa gharama. Kuliamsha Dreamliner letu kutua Marekani ni gharama kubwa lakini kama ni kweli tumedhamiria kwa dhati kuutangaza utalii wetu kimataifa, hatuwezi kukwepa gharama. Lazima tutangaze vivutio vyetu kimataifa na namna bora ya kujitangaza kimataifa ni kupitia usafiri wa ndege wa kimataifa.

Tanzania na Marekani, tuna mkataba wa anga huria, hivyo hatuhitaji kuomba haki za kutua kwenye viwanja vyovyote vya Marekani. Tunachohitaji ni kutoa tu taarifa ili tutengewe eneo la kuegesha ndege yetu.

Dreamliner yetu Boeing 787 - 8 inabeba abiria 248 yaani abiria ni 240 na wafanyakazi wanane. Tukiweka akiba ya nafasi 40 kwa Rais na ujumbe wake, halafu tukabeba abiria 200, kila abiria alipe kiwango fulani cha nauli ili kumsindikiza Mama kuzindua Royal Tour, Watanzania wakihamasishwa tu, hata wasanii tu wa Bongo Movies na Bongo Fleva wangeweza kuijaza.

Ukijumlisha na wafanyabiashara tungeweza hata kufikisha abiria 500. Nimeshuhudia kwenye Dubai Expo, mbona tuliweza?

Hatua hiyo ingeleta maana ya kweli na halisi ya uzinduzi huo wa Royal Tour nchini Marekani, kama Rais Samia angetua kwa Dreamliner na ATC kuzindua safari za moja kwa moja kutoka Marekani.

Hakuna kitu kizuri kama Rais Samia angetua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa JF Kenedy (JFK) kwa Dreamliner na kupokewa uwanjani hapo na Watanzania waishio Marekani kisha kwenda naye hadi hotel aliyofikia.

Nikisema Watanzania ni wavivu katika kuchangamkia fursa, nitakuwa ninawaonea? Kama ndege tunazo, abiria tunao na soko lipo, hivi tuliinunua hii midege ya nini?.

Kweli ATC wanaona raha hii midege ya masafa marefu ikiruka na kutua katika viwanja vya ndani huku ikibeba vile vindoo vya samaki sato kutoka Mwanza kwenda Dar es Salaam na KIA pekee?. Tukisema pamoja na mambo mengine yote, shirika letu la ndege kuendelea kupata hasara mwaka hadi mwaka kunachangiwa na kukosekana kwa wataalamu wa kufikiri na kupanga mikakati (strategic thinking and planning) kwenye biashara ya usafiri wa anga tutakuwa tunakosea?

Nawatakia uzinduzi mwema wa Royal Tour hapo kesho na Pasaka Njema

**Wasalaam.**
**Paskali (alizaliwa siku ya Pasaka).**
**255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mitaa iitwe majina ya kihistoria si uswahiba



Na Joseph Kulangwa

**Wachache sana tena matajiri, ndio walikuwa na uwezo na msuli wa kuwa na simu nyumbani kwao, vinginevyo mpaka kuche uwe ofisini na uwasiliane na opareta ndipo ujue unawasiliana na nani tena kwa muda gani.**

HAKUNA kitu kizuri kama kujua ndugu au rafiki yako yuko wapi na anapatikanaje, unapomhitaji kwa mema na mabaya pia. Anwani inasaidia sana kumpata ndugu huyo au hata kumfikishia ujumbe na mzigo wowote unaotaka umfikie.

Zamani enzi kabla ya kuwa na simu janja, tulitumia simu za mezani tena za kukoroga na wakati mwingine ilibidi mtu upitie kwa opareta ili kumpata mtu wako unayetaka kuwasiliana naye.

Lakini leo hata kama umelala nyumbani kwako, unaweza kumtafuta mwenza wako ukampata mkazungumza mnavyotaka ili mradi kifurushi chako cha bando kinakuruhusu. Enzi hizo mpaka uwe ofisini ndipo uongee na mtu wako.

Wachache sana tena matajiri, ndio walikuwa na uwezo na msuli wa kuwa na simu nyumbani kwao, vinginevyo mpaka kuche uwe ofisini na uwasiliane na opareta ndipo ujue unawasiliana na nani tena kwa muda gani.

Enzi hizo ulizungumza kwa malipo, hivyo kwa muda, na ukiisha simu inakatika unasubiri kuomba upya ili uunganishiwe na wakati mwingine ukiomba alipe unayempigia, na hasa akiwa ni bosi kakutuma kumletea taarifa.

Hili la anwani za makazi ni zuri sana kwamba sasa itakuwa rahisi kujua nani anaishi wapi na nyumba ipi, hivyo hata mawasiliano kwa magari na pikipiki inakuwa rahisi. Bodaboda unamwambia peleka hiki mtaa fulani nyumba fulani. Mwaminifu anafikisha.

Namfuatilia sana Waziri wetu wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, anauchapa mwingi kwa kuzunguka karibu nchi nzima kuhamasisha hilo, ingawa wakati mwingine naona lina gharama zisizo za lazima.

Tuache hayo, gharama anajua anayetaka lifanikiwe. Inawezekana kweli kuna gharama halali. Mimi nasisitiza alilolisema Nape, kuhusu majina ya mitaa husika. Anasema lazima tuwe na majina ya kihistoria.

Hapo kama ni mlenga shabaha kapiga kwenyewe, kwenye wanakoita 'bull', kalenga haswa, kwamba tutumie fursa hii kuwakumbuka wahenga wetu waliolitoa huko Taifa hili na kulifikisha hapa lilipo.

Wapo watu wengi mashuhuri katika historia ya nchi hii ambao mpaka sasa wamesahaulika kwa makusudi au kwa bahati mbaya, hao safari hii tuwakumbuke, waonekane kwenye mitaa yetu badala ya kubuni majina bora majina.

Nakumbuka mwaka fulani wa hivi karibuni, wakazi fulani wa mtaa fulani Kinondoni, Dar es Salaam, wakajiamulia na kuandika jina la Victor Wanyama, Mkenya anayecheza soka la kulipwa Uingereza, eti akapewa mtaa!

Kwa nini? Sijui, lakini walikuwa wanajua hao wenye mtaa wao, ila kukaibuka ubishani na upinzani, nadhani bango hilo likaangushwa na hivyo jina la mwanasoka huyo likapotea. Nikajiuliza kama walitaka majina ya wacheza soka, Gibson Sembuli lipo.

Kina Maulid Dilunga hata Abdallah Kibadeni waliopata kuchaguliwa kuchezea timu ya Afrika kwa nini wasipewe mitaa badala ya kuitupa kwa watu ambao hatuna historia nao? Nape nampa alama zote kwa hili.

Tuache tabia ya kuita mitaa majina ya marafiki au washikaji zetu, yasiyo na historia wala mchango uliotukuka kwa jamii ya Watanzania hawa hasa wakazi wa maeneo husika eti tumpe huyu kwa kuwa ni tajiri! Hapana!

Tusirudi tulikotoka, kwa madaraja na barabara kupewa majina ya watu kwa kuangaliana uso na sura au uswahiba! Najiuliza kila siku, hivi kweli lile daraja la Tazara kuitwa Patrick Mfugale! Barabara la Chamwino Dodoma, kuitwa Patrick Mfugale! Jengo la uwanja wa ndege Chato, Geita kuitwa Mfugale Tower!

Tukae chini bila kutazamana makunyanzi, lile daraja la Ubungo kuitwa John Kijazi kweli? Soko Kuu la Dodoma kuitwa la Ndugai kweli? Kwa lipi? Liko wapi la Chifu Adam Sapi Mkwawa? La Pius Msekwa? La Samuel Sitta? La Anne Makinda? Kwa nini Ndugai? Wote hawa maspika au siyo? Kama ndiyo kwa nini sasa?

Tuwe makini katika kutafuta majina ya barabara na mitaa yetu ili iwe sehemu ya kujifunza Historia kwa vizazi vya sasa na vijavyo, lakini pia kama sehemu ya utalii. Kwamba huu mtaa unaitwa Mama Maria Nyerere na sababu zipo. Au siyo? Alamsiki!

SAFU

# FAHAMU ATHARI ZA UMBEA, MAJUNGU KATIKA FAMILIA NA MAENEO YA KAZI

## DARASA LA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**"Umbea na majungu ni dalili ya mtu au kikundi cha watu kufilisika kifikra na kimawazo. Vitu hivi ni hatari kwa amani na mshikamano katika familia na jamii kwani huchochea vurugu, fujo, mpasuko wa kifamilia na kijamii.**



TUNAISHI katika jamii ambayo ubinadamu unatawala hali ya kiMungu ndani ya binadamu na watu wengi wamejeruhi wenzao kwa sababu ya umbea na majungu.

Katika kipindi hiki ambacho jamii inapambana na ugonjwa wa UVIKO- 19, manyanyaso, dhuluma, ukatili wa kijinsia na maadui wengine, hakuna budi kupambana na adui umbea na majungu, kwani mambo haya yamewajeruhi watu, kuvuruga watu na kusababisha vifo katika jamii.

Ni wakati mwafaka, katika kupambana na maadui hao umbeya na majungu, jamii kutafakari na kujiuliza pasipo aibu na kujihurumia ni kwa jinsi gani mtu anatumia silaha za umbea na majungu kujeruhi wengine.

Umbea na majungu ni dhambi kama dhambi zingine. Mambo hayo ni uovu, ubinafsi, aina ya ugaidi, upagani; ni kupoteza imani na upendo kwa mtu husika na kwa watu wengine. Umbea na majungu ni dhambi kubwa kwa sababu huwajeruhi watu wengi, huharibu heshima na sifa za watu, huvunja uhusiano baina ya watu na marafiki, kuharibu kazi ya mtu, na kusambaratisha familia.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba umbea huzungumzwa kirahisi, husikilizwa kwa makini na kusambazwa kwa haraka sana. Mbaya zaidi, watu wengi huamini mambo ya umbea na majungu kuliko wanavyoweza kuamini mausia na mafundisho yenye kujenga.

Ugaidi wa umbea na majungu msingi wake ni ulimi. Wakati mwingine ulimi umetumika kusema uongo na kuchafua mtu au watu kwa lengo la kuharibu. Mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari wakati mwingine vimetumika kusambaza habari za uongo na kuchafua watu.

Ni dhahiri kwamba mtu mmoja anapochafuliwa, hali hiyo haimhusu yeye tu bali familia yake, wazazi wake, ndugu zake na watu wengine wanaomtegemea. Mtu mmbea na mpiga majungu ni gaidi anayewaangamiza watu wengine. Kwa maneno mengine, umbeya na majungu vimesababisha kusambaratika na kugawanyika kwa watu katika jamii hata kusababisha ukosefu wa amani na hata baadhi ya watu kupoteza maisha.

Umbea na majungu, wivu, husuda na chuki, hujibainisha katika kutothamini kazi nzuri za watu wengine, kupinga sifa zitolewazo kwa mema waliyotenda ili kuhalalisha uzushi na kumdhalilisha mtu mwingine.

Katika jamii ya sasa, wako watu ambao kazi yao ni kufitinisha watu wengine kwa kutafuta na kusafirisha habari. Watu wa aina hii hupenda kusikia mambo ya wengine na kuyapeleka kwa wengine, jambo ambalo huvuruga amani na mshikamano katika familia na jamii.

Umbeya na majungu ni dalili ya mtu au kikundi cha watu kufilisika kifikra na kimawazo. Vitu hivi ni hatari kwa amani na mshikamano katika familia na jamii kwani huchochea vurugu, fujo, mpasuko wa kifamilia na kijamii.

Ili kuleta afya, ustawi na maendeleo katika jamii husika, kila mtu anapaswa kuwafikiria na kuwanenea watu wengine mema kwa kuwa wema na ubaya ni akiba. Watu wasiendekeze umbea na majungu dhidi ya wale ambao hawawapendi au hawaelewani nao au wanaojisikia kuwa wanyonge kwao.

Ni vizuri na ni ucha Mungu kukabiliana na mtu uso kwa uso au ikibidi kutumia mtu mwingine mwenye hekima kutafuta suluhu kadri ya busara na hekima itokanayo na upendo. Ni vyema kuwaheshimu watu wengine. Pia ni vibaya kuwatendea wengine yale ambayo hupendi kutendewa. Apandaye mbegu ya fitina, atavuna zao la fitina yake.

Jambo la msingi na jamii inapaswa kufahamu ni kwamba ni vibaya kusema jambo kuhusu mtu mwingine kwa kile ambacho huna ujasiri wa kusema mtu huyo akiwa mbele yako.

Mtu awanenee wengine yale apendayo wamseme yeye.

Kadhalika, mtu anaposikia mambo ya umbea, asiyafurahie wala kuyachangamkia ili asishiriki dhambi hiyo. Mmbea na mpiga majungu anapoanza kusema mambo yake mkanye, mwelimishe au badili mazungumzo au onesha kutokujali. Jenga ukuta mkubwa masikioni mwako dhidi ya umbea, majungu na uzushi.

Busara na hekima ya maisha inawataka watu kuzuia midomo yao, kutawala ndimi zao na kuepuka fitina. Wakati wote, mtu anayeeleza mambo yako kwa wengine, akifika kwao ataongea mambo yako pia. Umbea na majungu imekuwa silaha ya watu waoga na dhaifu ambao hawathubutu kukabiliana na watu ambao wanahisi kutokuelewana nao au waliowazidi uwezo.

**UMBEYA KICHAKA**

Aidha, umbea na majungu ni kichaka na maficho ya watu wavivu katika wajibu na kazi. Watu wa aina hii hawana muda wa kuchosha akili zao kufikiri na kubuni mambo yenye tija. Hivyo, dhamiri zao zinawasuta wanapoona wengine wakifanikiwa au kusifiwa kwa kazi njema.


Uhusiano mbaya baina ya dunia na wakaaji wake, baina ya Mungu na watu wake, baina ya ndugu na ndugu, waumini kwa waumini na watumishi kwa watumishi na ni matokeo ya tamaa ya vitu, hali, hadhi na heshima ambayo inaibua na kuchochea hali ya wivu, chuki na husuda inayojieleza na kujipambanua katika umbea na majungu. Umbea na majungu ni mtaji wa watu dhaifu na wasiojitambua.

**"Umbea na majungu ni kichaka na maficho ya watu wavivu katika wajibu na kazi. Watu wa aina hii hawana muda wa kuchosha akili zao kufikiri na kubuni mambo yenye tija."**

Viongozi katika ngazi ya familia, jamii na maeneo ya kazi wanapaswa kuwa sehemu ya suluhu na si tatizo. Viongozi wanapaswa kuwa sababu ya kuleta uponyaji katika dunia dhidi ya hali hii ya ugaidi wa umbea, majungu, uzushi na fitina.

Katika nafasi walizo nazo, viongozi wana wajibu wa kujenga uhusiano bora baina ya muumba na viumbe, baina ya watu na viumbe. Viongozi kujiingiza katika umbea na majungu ni kujikosea na kuwakosea wanaowaongoza. Viongozi wanapaswa kuwa wapatanishi na watafuta maridhiano na suluhu juu ya changamoto.

Tunapoadhimisha ya Pasaka na kuendelea na mfungo Mtukufu wa Ramadhan, watu wanapaswa kukumbatia upendo, utu wema na fadhili na utayari wa kutenda mema kwa binadamu mwingine ili Mungu atutakabali.



**■ Mch. Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

APRILI 17, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 13


**Vazi pendwa kwa vijana wa kisasa**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Nyumba yako inaonekana vipi wakati wa sikukuu?



Ukurasa 12

**HARUSI**




**VIUNGO VYA JIKONI**


# Vinavyokupa mng'ao mwanana

Ukurasa 14

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | T | A | M | B | O |
| | A | | | A | |
| O | K | A | | N | |
| | A | | O | D | A |
| | S | | | U | |
| B | A | N | D | A | |





## PAKA RANGI




### FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
UDA, BAA, TAMKA, SANDA, DANDIA, SHAMBA

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa akijisomea kitabu chache cha shule chini ya mwembe uliokuwa pembeni ya nyumba yao. Wakati akiendelea kusoma, mara alipita mzee mmoja akiuza mikeka, vikapu na misala.

Alimuona mzee huyo akipita, alimwita mama yake aje haraka pale alipokuwa amekaa.

**Juma:** Mama njoo kuna misala inapita.

**Mama:** Wee Juma acha kunisumbua mimi namalizia kupika

**Juma:** Lakini mama mwalimu alituambia kuwa Usiache ambachao kwa msala upitao, ndo maana nikakuita.

**Mama:** Sasa huo msemo una maana gani hapa? Mwalimu wako alimaanisha kwamba usiache vitu vyako ulivyovizoea kwa mambo ya kupita na sio vinginevyo.

**Juma:** Kumbe mama nimekuelewa

**SWALI**

Kenge na mjusi wapo katika kundi gani la wanyama?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mbona wasipoona kwa macho hawaamini?

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na mada zetu. Bado tunajadili kuhusu imani. Nikanukuu neno la Mungu kwamba Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Nikaanza kuelezea imani ambayo ni macho yako ya kiroho inavyopatikana.***

Chanzo cha imani ni kumwamini Mungu. Na ili umwamini Mungu ni lazima umwombe Roho Mtakatifu akuwezeshe kumwamini Mungu. Hatumwamini Mungu kwa sababu tu tumeamua kumwamini. Imani huumbwa ndani yetu na Roho wa Mungu kwa wale wenye kiu hiyo.

Yakupasa pia kutambua kwamba wewe ni mtoto wa Mungu. Kujitambua hivyo kutaimarisha macho yako ya kiroho ya kukupa uhakika wa mafanikio katika maisha yako!

Kutambua ukweli huu kutaimarisha imani itendayo kazi ndani yako na kukupa mafanikio Mungu aliyoyakusudia tangu mwanzo. Wewe ni wa kipekee sana hapa duniani miongoni mwa watu wote. Hakuna anayefanana na wewe na wala baada yako hatazaliwa wa kufanana na wewe.

Hukuzaliwa kwa kubahatisha, ulizaliwa kwa ridhaa ya Mungu na ndiye aliyekutayarishia mpango wa mafanikio katika maisha yako. Mungu haoni haya kukuita mtoto wake hata kama watu watakudharau au kukupuuza.

Kulitambua hili kutaendelea kukupa ujasiri wa kufanikiwa. Mtoto wa Mungu akitembea katika maono aliyopewa na Baba yake hashindwi; anaweza kujikwaa lakini hataanguka, anaweza kuchelewa lakini atafika.

Pia jenga tabia ya kuzungumza na Mungu. Tabia hii itaimarisha imani itendayo kazi ndani yako. Huwezi kudumu katika kumwamini Mungu usiyezungumza naye mara kwa mara.

Mtu ukizungumza naye mara kwa mara utafanana naye kwa tabia, hivyo kuzungumza na Mungu mara kwa mara kutakupa tabia na hali ya uungu ndani yako nasi tunajua Mungu hashindwi.

Wengi wetu tumesongwa na mahangaiko ya dunia, kukimbizana na biashara, huduma au masomo kiasi cha kukosa nafasi ya kuzungumza na Baba yetu. Tuna hofu za madeni, magonjwa, kufilisika, kufeli masomo, na hata kukataliwa kiasi kwamba Mungu amewekwa pembeni.

Kwa kadiri unavyokaa mbali na Mungu ndivyo imani yako inavyopungua na hatimaye kutoweka kabisa. Ninaposema jenga tabia ya kuzungumza na Baba hii ni zaidi ya kufanya maombi, yeye mwenyewe anasema; "Haya, njoo, tusemezane, asema Bwana". Mungu atatoa mwaliko kwako wa kuzungumza naye na katika mazungumzo hayo huwa ni ya pande mbili.

Vilevile, watumishi na viongozi wa dini Mungu amewatumia kuimarisha imani za watoto wake na kuwapatia mafanikio katika changamoto nyingi wanazokumbana nazo katika maisha.

Mwanamke mmoja aliachiwa madeni na mume wake aliyefariki dunia. Hali ya maisha ilikuwa ngumu na kumfanya ashindwe kulipa deni hilo. Hatimaye wadeni wakaja wakiwa na nia ya kuuza watoto wake ili walipwe. Kufika hapo mama yule imani iliporomoka na hakuona msaada mahali popote.

Ikatokea mtumishi wa Mungu kuitembelea familia hiyo. Alipusikia kilio chake akamwuliza amfanyie nini? Niambie una kitu gani nyumbani? Akajibu sina kitu ila chupa ya mafuta. Kwa macho ya kiroho mtumishi huyo aliona fursa ya kulipa lile deni kupitia yale mafuta.

> **Vilevile, watumishi na viongozi wa dini Mungu amewatumia kuimarisha imani za watoto wake na kuwapatia mafanikio katika changamoto nyingi wanazokumbana nazo katika maisha.**

Akamwagiza mama kwenda kutaka vyombo vingi vitupu kwa jirani, kisha aingie ndani ajifungie na wanawe akavimiminie mafuta vyombo vyote. Vilipojaa vyote mtumishi huyo akamwambia mama akayauze mafuta yale aweze kulipa deni lake!

Eneo lingine unalopaswa kujielekeza katika kuimarisha imani yako ni kujenga tabia ya kulisoma neno la Mungu. Wapo watu walioimarisha imani zao na hatimaye kupata mafanikio makubwa.

Kijana mmoja alimkasirikia babu yake kwa kumzawadia Biblia kama zawadi siku yake ya kuzaliwa. Akakata mawasiliano naye mpaka babu alipofariki dunia. Siku ya mazishi akakumbuka ile Biblia aliyopewa, akaichukua ili apate neno la kwenda kusoma kwenye ibada ya mazishi.

Alipofungua Biblia ikadondoka hundi iliyoandikwa Dola 30,000 yenye tarehe ile akisherehekea siku yake ya kuzaliwa. Babu alimwandikia hundi ili akanunue gari kama zawadi, sharti ni kusoma Biblia. Imeandikwa, "Basi imani, chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Mungu".

Tuishie hapa, wiki ijayo tuang***alie mambo yanayoua imani za wengi. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Tutunze misitu, kuongeza nishati jadidifu kuokoa mazingira

WIKI iliyopita, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitangaza kupungua kwa mvua za masika kutokana na kubadilika kwa mwelekeo wa upepo baharini huku sababu kubwa ikielezwa ni mabadiliko ya tabianchi.

Kwa ujumla, mabadiliko ya tabianchi yamesababisha mvua kupungua, kunyesha zenye kuleta majanga makubwa kama mafuriko na uharibifu wa mali kiasi cha watu kupoteza maisha.

Kutokana na hali hiyo, wakulima wameshauriwa kulima mazao yanayohimili ukame maana yake hakuna matarajio ya kupata mahindi au mazao mengine ya muda mrefu, hali ambayo itaathiri upatikanaji wa chakula.

Hii inatuma salamu kwa kila binadamu kwamba zinahitajika jitihada za makusudi kulinda misitu, kupanda miti na kuacha uharibifu wa mazingira ambao kimsingi ni kichocheo kikubwa cha mabadiliko hayo.

Tanzania imejaliwa kuwa na misitu ya asili na kupanda pamoja na maeneo yaliyohifadhiwa au kila mtu kupanda miti kwa kadri ya anavyoona umuhimu.

Misitu huchangia kuvuta mvua, husaidia kunyonya hewa ukaa (chafu) inayozalishwa na shughuli za kibinadamu kama viwanda na magari yanayotumia petroli na dizeli ambayo ndiyo mengi.

Ni nadra sana kusikia watu wakizungumzia umuhimu wa kutunza misitu kama rasilimali muhimu ya kuwasaidia kujikwamua kiuchumi kwa kuwa kupitia misitu viko vijiji vinaingiza mamilioni ya fedha kwa kadri eneo lao lilivyopunguza hewa ukaa angani.

Faida nyingine ya misitu ni jamii kupata mahitaji kama kuni, dawa, mbao, magogo na mazao mengine ya misitu ambayo huwaingizia kipato na kuwawezesha kuishi kwa urahisi zaidi. Maana yake inapokwisha, inapunguza au kuondoa kipato cha watu.

Kwa hali ilivyo, imechangia kupungua kwa mvua, kiasi cha maji kwenye vyanzo mbalimbali hadi baadhi ya mamlaka za maji kutangaza mgao wa rasilimali hiyo,ni lazima kulinda misitu na kuongeza kasi ya kupanda miti.

Misitu inakwisha kwa kasi kutokana na shughuli kama za kuvuna kwa ajili ya mkaa kwamba watu wanataka wapate kipato pasipokuwa na mpango endelevu wa kutunza rasilimali hiyo ni lazima kuwa na mkakati wa kuvuna.

Kwa sasa nishati ya gesi imepanda bei kiasi kwamba kasi ya kutumia mkaa imerudi kama kawaida, maana yake idadi ya miti inayovunwa inaongezeka.

Tunajua mti unaotoa mkaa mzuri ni uliokomaa vizuri maana yake ulipandwa miaka zaidi ya kumi iliyopita, unapoukata leo na kupanda mwingine maana yake kuna kazi ya ziada ya kuusubiri hadi ufae kuvunwa jambo ambalo halifanyiki hivyo.

Ni lazima serikali iongeze kasi ya kulinda misitu hasa kwa kujenga mazingira rahisi kwa wawekezaji wa nishati mbadala yaani nishati jadidifu ambayo hutunza mazingira kwa kuwa wananchi wakiwa na uhakika wa nishati maana yake watatunza mazingira.

Tanzania tumejaliwa maeneo yenye kuwezesha kuzalisha nishati jadidifu kama vile upepo,jua na joto ardhi ambazo zikivunwa ipasavyo tutaondokana na matumizi ya umeme wa maji ambao kwa kiasi kikubwa unaathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi.

Mara kadhaa wawekezaji wamepaza sauti juu ya utitiri wa vibali vinavyopatikana maeneo tofauti, wanalazimika kusafiri kwenda Dar es Salaam au Dodoma au mikoani miradi ilipo ili kuomba vibali maana yake wanatumia muda mwingi na fedha nyingi.

Ni lazima jitihada za kutunza mazingira zikaenda pamoja kwa kuangalia namna gani nchi itazalisha nishati jadidifu ambayo itatumiwa na wananchi waachane na matumizi ya mkaa ambayo kimsingi yanateketeza misitu.

Unaposafiri kwenda mikoa mbalimbali utaona maeneo yanavyozidi kuharibiwa kwa uvunaji wa misitu usio endelevu, lakini unaposafiri kwenda nje ya Dar es Salaam kwa nia yoyote utakutana na magari na pikipiki zimebeba mkaa unaoletwa mjini kwa ajili ya nishati.

Kuna wakati serikali ilizitaka taasisi kama shule na magereza ambazo hutumia kuni nyingi kuanza kutumia gesi kwa ajili ya kupikia,lakini utekelezaji umekuwa mgumu hadi sasa tani kwa tani za kuni hupelekwa kwenye haya maeneo.

Bila kuchukua hatua madhubuti kwa serikali kuhakikisha nishati inapatikana kwa bei rahisi ni ngumu sana kuzuia uharibifu wa mazingira, itakuwa kuongea majukwaani lakini utekelezaji unakuwa mgumu kwa kuwa watu hawana nishati mbadala kwa ajili ya shughuli nyumbani.

Tanzania ilivyoanza kuzalisha gesi asilia maarufu kama gesi ya Mtwara, waliaminishwa itasambazwa nyumbani kama maji kwamba watu wataipata kwa bei rahisi lakini hadi sasa mradi huo haujafikia robo ya nyumba za Dar es Salaam, jambo linalotaka mamlaka kuamka na kufanya kazi ya ziada kuhakikisha nishati inapatikana.

Bila kutafuta nishati jadidifu kwa wananchi utunzaji wa mazingira wa kuandika kwenye ripoti na kuongea jukwaani itakuwa ni kazi bure kwa kuwa misitu inazidi kuteketea na madhara ndiyo tunayaona kama sasa mvua hazinyeshi kwa wakati au zimepungua na kupungua kwa maji kwenye vyanzo mbalimbali.

# HARUSI







Picha tofauti za msemaji wa klabu ya Yanga, Haji Manara baada ya kuoa mke wa pili Rubynah Salum, harusi hiyo imefanyika wiki hii.







# MITINDO

## SURUALI ZA KUBANA






# Vazi pendwa kwa vijana wa kisasa

KUVAA nguo nzuri zenye mitindo ya kisasa ni sehemu ya maisha ya kila siku kwa vijana wengi wa kike na wakiume.

Kutokana na aina hizo za nguo kuwa pendwa, wabunifu na viwanda vya kutengeneza nguo vinashindana kutoa matoleo mapya ili kukabiliana na mahitaji ya soko.

Siku hizi ni kawaida kumuona mtu akiwa amevaa shati, fulana na suruali zote zikiwa zimembana mwili, kimtizamo anakuwa na mvuto wa kipekee.

Hata hivyo, wachambuzi wa mavazi wanasema mitindo ya nguo za kubana siyo mipya, ilikuwa inatumiwa zamani lakini ya sasa imeboreshwa kwa kuongezewa vikorombwezo mbalimbali vinavyovutia.

Mchambuzi wa masuala ya mavazi, anasema suruali za kubana ni mtindo wa zamani ambao umerudi kwa kasi, hasa kupitia suruali aina ya jinsi, huko zamani zilikuwa zikiitwa 'Chupa'.

Suruali za kubana mwanzoni zilivaliwa na wanasiasa wa kundi la mrengo wa kushoto la Sans-culottes, ambao walikuwa wapinzani wakubwa wakati wa Mapinduzi ya Ufaransa, wakati huo suruali hizo waliziita 'pantaloons'.


Uvaaji huo ulianza kama uasi na kuwa mtindo wenye umaarufu katika miaka ya 1950. Suruali hizo baadaye zikaanza kuvaliwa na mastaa wa rock'n'roll katika miaka ya 1960 na kuendelea kusambaa katika jamii.

Katika mabadiliko hayo, sasa suruali za kubana zipo za aina nyingi ikiwamo zile za vitambaa.

Imekuwa kama jambo la kishamba pale kijana akionekana akiwa amevaa nguo za kawaida.

Pamoja na mwonekano wake mzuri, lakini wataalamu wanaonya wanasema endapo mtu akipenda kuvaa suruali ya kubana kila wakati, kuna hatari ya kupata madhara kama kupungukiwa na nguvu za kiume kutokana na mishipa ya fahamu kubanwa.

UREMBO



VIUNGO VYA JIKONI

# Vinavyokupa mng'ao mwanana

UZURI wa ngozi sio rangi tu bali ni muonekano wake wenye mng'ao unaoashiria afya njema.

Kufanya tiba mbadala kwa kutumia vitu vya jikoni, unaweza kuimarisha ngozi kuwa nzuri, laini na yenye mng'ao wa kipekee.

Tiba hii unaweza kuifanya mara moja kwa wiki au mara moja ndani ya wiki mbili, inategemea na nafasi yako lakini matokeo mazuri lazima uyapate haraka.

**MAHITAJI**

Kiini cha yai, machicha ya nazi, tango au limao.

**JINSI YA KUANDAA**

Safisha uso wako kwa maji safi ya vuguvugu.

Kama una ngozi kavu au ya kati chukua kipande cha tango kidogo na upake maji yake usoni.

Kwa wenye ngozi ya mafuta unaweza kutumia kipande cha limao kwa kupaka maji yake.

Kisha chukua pamba au kitambaa laini na futa maji ya tango au limao usoni taratibu.

Chukua machicha ya nazi na anza kuusugua uso na shingoni taratibu mpaka uridhike uso wote umepitiwa na machicha yako hasa unapoona unang'aa kwa mafuta kidogo yaliyotoka kwenye nazi.

Halafu ondoa machicha ubaki na uso unaong'aa bila vitu vyeupe yaani machicha.

Chukua kiini cha yai la kienyeji, au la kisasa lenye kiini cha njano iliyokolea. Hakikisha kiini kisijichanganye na ute wakati wa kupasua, limimine kwenye sahani ambayo unaona kiini katikati kisha unakichota na kuweka kando.

Paka ule uji mzito wa njano wa kiini uso mzima bila kusahau shingoni na nyuma ya masikio na ngozi ya masikio. Baada ya kupaka kiini cha yai unaweza kuendelea na shughuli zako huku likiendelea kukauka, inapokauka ngozi yako inakuwa kama inajivuta vuta.

Osha uso wako kwa maji safi na maji yawe ya baridi sasa.

**UMUHIMU WAKE**

Kuosha uso kwa maji ya vuguvugu hufungua matundu ya ngozi.Tango au limao hutumika kama kisafisha ngozi na unapojifuta taratibu unaondoa uchafu katika ngozi yako.

Machicha ya nazi yanatumika kama kikandio cha kuondoa seli zilizokufa, kuifanya ngozi kuwa laini na kupa mng'ao. Kiini cha yai hapa kinatumika kama maski, matundu ya ngozi yanajifunga vizuri na kinaipa ngozi yako lishe kutokana na vitamins zilizomo kwenye kiini cha yai kama vitamin E.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Minofu ya kuku inapendeza sikukuu

NYAMA hii ya kuku inapikwa kwa muda mfupi, lakini matokeo yake ni mazuri mno.

Ni chakula muafaka kuandaa wakati wa mwishoni mwa wiki au hasa wakati wa sikukuu ili uweze kuondoa msongo wa mawazo kwa mlo safi.

Minofu ya kuku nusu kilo na unaweza kuandaa kiasi kinachotosha, asali vijiko vinne vikubwa, sukari ya brown kijiko na nusu vikubwa, Soy Sauce nusu kikombe, sawa na vijiko vinne vikubwa.

Tangawizi iliyosagwa vijiko viwili vidogo, kitunguu saumu kilichopondwa vijiko viwili vidogo, chilli sauce vijiko vitatu vikubwa, chumvi nusu kijiko kidogo, cayenne pepper kiasi, mafuta ya kula, tumia mafuta ya zaituni vijiko 5 vikubwa, currypowder kijiko kimoja cha chai, na ndimu moja.

**NAMNA YA KUANDAA**

Kwenye bakuli safi, changanya pamoja sukari, asali, soy sauce, tangawizi, kitunguu saumu, currypowder, coriander powder na chilli sauce.



Koroga hadi vichanganyike vizuri na hifadhi mchanganyiko pembeni.

Andaa safisha minofu ya kuku, kausha maji, kata vipande vidogo kisha hifadhi kwenye chombo safi. Nyunyizia chumvi, cayenne pepper na ndimu kiasi kisha changanya ili vipate kuenea vizuri.

Hakikisha kuwa ni minofu na imekatwa vipande vyembamba na vidogo ili viive vizuri na haraka.

Bandika sufuria jikoni, hakikisha moto uwe mkali . Weka mafuta ya kula kiasi kidogo, yakipata moto weka minofu ya kuku.

Acha upande mmoja uive vizuri kwa muda wa dakika moja hadi mbili, kisha geuza upande wa pili. Hakikisha nyama haiungui. Upande wa pili ukishaiva toa nyama weka pembeni.

Awamu ya mwisho ya nyama ikishaiva, usitoe kwenye sufuria, bali chukua nyama iliyoiva weka tena. Geuza kwa pamoja kisha mwagia sauce uliyoandaa na koroga vizuri ili ichanganyike na nyama.

Hakikisha huachi kukoroga hadi sauce iwe inanata na imekuwa nzito. Hapo kuku wako atakuwa tayari.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Nyumba yako inaonekana vipi wakati wa sikukuu?

MSIMU wa sikukuu umewadia huku kukiwa na pilikapilika za hapa na pale katika nyumba kukiwa kunaonekana kutawala mapambo yanayoshabihiana na msimu wenyewe.

Katika makala hii ya nyumba, tunaweka dondoo kidogo kukuongezea baadhi ya vitu ambavyo vitasaidia kuifanya sikukuu yako kuwa nzuri, ukaifurahia ukiwa nyumbani kwako.

Naamini kwamba kipindi hiki familia nyingi huwa zinaungana pamoja katika mapumziko. Kwa hiyo ni muhimu kukifanya kipindi hiki kikawa ni cha furaha zaidi nyumbani.

Katika kipindi hiki ni muhimu nyumba ikawa na vionjo tofauti hususani mapambo yenye kumbukumbu ya kifamilia ambayo pia yanachangia kuleta furaha katika kipindi hiki ambacho familia imejumuika pamoja nyumbani.





Unaweza kuchanganya na mapambo mengine tofauti kama 'wall papers' na mengine kwa kuzingatia rangi zinazoshabihiana na sikukuu pamoja na maua ya kawaida au ukaweka kumbukumbu ya picha za pamoja za familia kama zipo.

Mapambo mengine ambayo unaweza kutengeneza ni ya maua ya asili kwa kuyaweka katika chupa au chombo maalum ambacho kinaweza kuwekwa hata juu ya meza.

Pamoja na kupendezesha nyumba, pia hewa na harufu hubadilika na kuwa nzuri zaidi kutokana na maua yanayowekwa ndani.

Pia unaweza kutengeneza maneno yenye ujumbe maalum kwa kuyaandika mwenyewe ya kuendana na msimu au ukayanunua katika sehemu maalum yanapopatikana na kuyaweka nyumbani kwako.

Hakikisha unaweka mapambo sehemu ambayo ni salama na hayawezi kuharibika kwa namna yoyote au kuharibiwa na watoto.

Vilevile, nyumba katika msimu huu inatakiwa iwe inapigwa nyimbo zinazoshabihiana na msimu wenyewe.

Baada ya kuisha kwa msimu wa sikukuu unatakiwa uyaondoe na kudizaini upya muonekano wa nyumba yako.

## Kuandaa meza ya siku ya kuzaliwa kwa vitu vya asili



SHEREHE ya kuzaliwa ni muhimu kwa kila mtu ili kumpatia furaha na faraja katika kukumbuka siku hiyo.

Wapo wanaofurahia siku hiyo wakiwa katika mahoteli ya kifahari, ndani ya boti na hata katika ukumbi ulioandaliwa vizuri.

Hata hivyo, unaweza kufurahia kumbukizi hiyo ukiwa nyumbani huku ukiwa umeipamba vyema meza ambayo itatumika kwa ajili ya kula keki na vyakula vitamu.

Leo nakupatia dondoo za namna ya kupamba meza ya siku ya kuzaliwa kwa kutumia vitu vya asili.


**1:** Pamba meza yako kwa vitambaa vya mchanganyiko wa rangi nyekundu na kijani ili kuifanya meza kuwa katika mazingira ya uhai zaidi.

**2:** Unaweza kuweka pia vitambaa vya leso pamoja na vifuniko vya mti wa mianzi kama mapambo ya mbao.Hapa unaweza kuchagua vyenye rangi nyekundu au kawaida.

**3:** Hakikisha kuweka utungaji mzuri wa matunda katikati ya meza ya sherehe kama mananasi, ndizi, maembe, zabibu, machungwa na tende.

**4:** Sahani zinazoonekana za asili na zisizo za kawaida kwenye meza ya sherehe ambazo kwa muonekano wake utawafanya watu kushangaa.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
NIMEMPIMA MKEO AMEMEZA 'GOOGLE' NDIO MAANA KILA UKICHEPUKA UNA-MSTUKIA KAFIKA!
SASA PASAKA YOTE HII NITULIE NYUMBANI INAWEZEKANAJE? MIE SIO KUFULI NNA ROHO.
JIRANI UMEYASIKIA MAPYA YALIYOTOKEA YUKRENI NA URUSI?
NIPE UBUYU! MANAKE JANA UMENAMBIA WAME-WEKA SILAHA CHINI NA KUANZA 'KUSUTANA!'
MH! HUU MWALIKO WA PASAKA UNA-MUSHKELI, NAWEZA KUAMBULIA KUNUSA CHUPA ZA BIA!
BABY ONDOA MKONO SHAVUNI UNANITIA UNYONGE MALIKIA WAKO!
WE UNAFIKIRI MAZURI KUIAGA FAMILIA YANGU NIPO 'SIMIYU KIKAZI' KUMBE NIPO MANZESE UMENIBANANISHA NA PASAKA YOTE HII?
ABIRIA TUTATUA URUSI KUJAZA 'WESE' KISHA TUTAPAA NA KUSHUKA 'YUKREINI' TUPATE CHAKULA NA KUINJOI MANDHARI..
WEEE BABA! RUBANI USITUTAFUTE LA ROHONI...KAMA KWELI UMEYAAMUA HAYO KWA SHINIKIZO LA 'MIBANGE YAKO' KATUSHUSHIE BAHARINI AU LENGA MLIMA TUPUMZIKE!
BILA KUISHI KIDIGITALI MAISHA UTAYAONA KAMA DOMO LINAKUZOMEA!
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UKIPENDA HATA UKIFUMANIA...KATAA, SEMA SIO YEYE



Wanajeshi wa Russia wakiwa katika msururu wa magari ya kijeshi mashariki mwa Ukraine na kuibua tishio la uwepo wa mashambulizi ya pili ya ardhini nchini humo. **PICHA: BBC**

# Russia yaionya Marekani na washirika wake Yatishia matokeo yasiyotabirika endapo.....

**KYIV,** UKRAINE

RUSSIA imeionya rasmi Marekani na mataifa mengine washirika dhidi ya kusambaza silaha kwa majeshi ya Ukraine.

Onyo hilo lilikuja katika barua rasmi ya kidiplomasia kutoka Russia, ambayo nakala yake imepitiwa na vyombo vya habari nchini Marekani.

Barua hiyo ya kidiplomasia ya kurasa mbili iliyotumwa kwa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani na ubalozi wa Russia uliopo Washington inaonya upelekaji na usambazaji wa shehena za silaha unaofanywa na Marekani na Nato.

"Zinaongeza mafuta katika mzozo wa Ukraine, na inaweza kusababisha kile wanadiplomasia wa Russia wanataja kuwa matokeo yasiyotabirika," ilisema .

Barua hiyo ilitumwa siku ya Jumanne, mara tu baada ya habari kuhusu kifurushi kipya cha msaada wa kijeshi wa Marekani kwa Ukraine kuvuja.

Saa chache tu baadaye Rais Biden, aliidhinisha usafirishaji wa msaada wa kijeshi wenye gharama ya dola milioni 800.

Silaha hizo ni pamoja na makombora ya masafa marefu kama vile howitzers kwa lengo la kulinganisha uwezo wa kijeshi wa Russia nchini Ukraine.

Ofisa mkuu wa utawala wa Marekani alinukuliwa akisema onyo hilo linaweza kuonekana kama makubaliano na Russia kwamba msaada wa kijeshi wa Marekani na Nato kwa Ukraine ulikuwa na ufanisi.

Sehemu ya kwanza ya shehena hii ya hivi punde inatarajiwa kuwasili Ukraine katika siku chache zijazo, huku vikosi vya Russia vikiendelea kujipanga mashariki mwa nchi hiyo, kabla ya kile kinachotarajiwa kuwa shambulio kubwa katika eneo linalozozaniwa la Donbas nchini Ukraine.

**BORIS JOHNSON AWEKEWA MARUFUKU YA KUINGIA RUSSIA**

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, amezuiwa kuingia Russia kutokana na msimamo wake wa uhasama kuhusu vita vya Ukraine.

Waziri wa Mambo ya Nje ya Uingereza, Liz Truss, alisema, waziri mkuu wa zamani Theresa May na waziri wa kwanza wa Scotland Nicola Sturgeon ni miongoni mwa wanachama 13 wa serikali ya Uingereza na wanasiasa waliozuiwa kuingia nchini humo.

Hatua hiyo ilichukuliwa kwa kuzingatia kuwepo na hali ya uhasama wa serikali ya Uingereza dhidi ya Russia, hasa kwa kuweka vikwazo dhidi ya maofisa wakuu wa nchi hiyo.

Wizara hiyo ilisema katika taarifa yake, kuwa itaongeza orodha hiyo hivi karibuni.

Russia tayari imemzuia Rais wa Marekani Joe Biden na maofisa wengine wengi wa Marekani kuingia nchini humo.

**ZAIDI YA RAIA 1900 WAMEUAWA UKRAINE-UN**

Umoja wa Mataifa umerekodi mauaji ya zaidi ya raia 1,900 tangu kuanza kwa uvamizi wa Russia nchini Ukraine, lakini ilionya kuwa takwimu halisi inaweza kuwa kubwa.

Kati ya watu 1,982 waliouawa kati ya Februari 24 na Aprili 14, 162 walikuwa watoto, ilisema Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kibinadamu (OHCHR).

Raia wengine 2,651 wamejeruhiwa, 256 kati yao wakiwa ni watoto.

Ilisema vifo vingi na majeraha vilisababishwa na makombora na mashambulizi ya angani.

Awali, Kamishna Mkuu wa Haki za Kibinadamu Michelle Bachelet, alielezea kushtushwa na ripoti za raia waliouawa katika mji wa Bucha, karibu na mji mkuu wa Kyiv.

Alisema mauaji hayo yalijibu maswali mazito na ya kutatanisha kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa uhalifu wa kivita na kutaka ushahidi uhifadhiwe.

**MOSVKA ILIPIGWA NA MAKOMBORA MAWILI**

Kama tulivyoripoti hapo awali, maofisa wa Marekani bila kutaja majina yao, walisema wanaamini kuwa meli ya kombora ya Russia ilipigwa na makombora mawili ya Neptune ya Ukraine na kulikuwa na maofisa wa nchi hiyo ndani ya meli hiyo ilipozama.

Russia ilisema meli ya Moskva, ilizama baada ya moto kuwaka ghafla.

Meli hiyo ya kivita iliyokuwa na wafanyakazi 510 ilikuwa ishara ya nguvu ya kijeshi ya Russia, ambayo iliongoza mashambulizi ya majini dhidi ya Ukraine.

Anton Gerashchenko, mshauri wa wizara ya mambo ya ndani ya Ukraine, alisema nahodha wa meli hiyo, Anton Kuprin, alifariki wakati wa mlipuko na moto kwenye meli.

**ZELENSKY AONYA JUU YA UWEZEKANO WA NYUKLIA**

Rais Volodymyr Zelensky alisema ulimwengu unapaswa kujiandaa kwa uwezekano wa shambulio la nyuklia kutoka Russia dhidi ya nchi yake.

Zelensky aliulizwa katika mahojiano ya CNN kuhusu iwapo alikuwa na wasiwasi kuhusu maoni ya hivi karibuni ya mkurugenzi wa CIA, ambaye alisema Russia inaweza kutumia silaha za nyuklia za kimkakati katika uvamizi wake.

"Sio mimi tu dunia nzima, nchi zote zinapaswa kuwa na wasiwasi kwa sababu inaweza kuwa si habari halisi, lakini inaweza kuwa ukweli," Zelensky alisema, akibadilisha kwa kifupi kuzungumza kwa Kiingereza kwa msisitizo.

"Tunapaswa kufikiria tusiogope, tusiogope lakini tuwe tayari," aliendelea.

"Lakini hilo sio swali kwa Ukraine sio tu kwa Ukraine lakini kwa ulimwengu wote, nadhani." alisisitiza

Mwezi uliopita, msemaji wa Ikulu ya Kremlin, alisema Russia itaamua tu kutumia silaha za nyuklia ikiwa itakabiliwa na tishio lililopo. Zelensky pia aliulizwa kuhusu kuzama kwa meli ya kivita ya Russia yenye thamani kubwa, Moskva, lakini alikuwa na wasiwasi kuhusu ripoti kwamba ilipigwa na makombora mawili ya Ukraine.

"Tunajua haipo tena, kwetu sisi ni silaha kali dhidi ya nchi yetu, hivyo kuzama kwake si janga kwetu. Silaha chache ambazo Shirikisho la Russia linatumia kushambulia nchi yetu, ni bora kwetu." alisema.

> "Zinaongeza mafuta katika mzozo wa Ukraine, na inaweza kusababisha kile wanadiplomasia wa Russia wanataja kuwa matokeo yasiyotabirika,"

## SAFU

### MAKALA

# MTI WANGU, TAIFA LANGU, UHAI WANGU



Na Magabilo Masambu - 0689157789

**Mongela alitoa maelekezo kwa maofisa elimu wote wa wilaya chini ya usimamizi wa ofisa elimu wa mkoa, kuhakikisha wanafunzi na walimu katika kila shule ya msingi na sekondari pamoja na vyuo, wanapanda miti kwa wingi kadri iwezekanavyo.**

MTI Wangu, Taifa Langu, Mazingira Yangu, ni kaulimbiu iliyotumika katika maadhimisho ya kilele cha upandaji wa miti mkoani Arusha, shughuli ambayo ilifanyika katika Shule ya Msingi Enaboishu Academy, yenye mchepuo wa Kiingereza ndani ya Halmashauri ya Arusha Wilaya ya Arumeru.

Shughuli hiyo ya upandaji miti ilifanyika Aprili 8, mwaka huu ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, na kuhudhuriwa na viongozi wengine katika mkoa na wilaya za mkoa huo. Katika shughuli hiyo, zaidi ya miti 300 ilipandwa katika eneo la shule hiyo ikiwa ni sehemu tu ya zaidi ya miti milioni mbili inayotarajiwa kupandwa mkoani hapa.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Mongela alitoa maelekezo kwa maofisa elimu wote wa wilaya chini ya usimamizi wa ofisa elimu wa mkoa, kuhakikisha wanafunzi na walimu katika kila shule ya msingi na sekondari pamoja na vyuo, wanapanda miti kwa wingi kadri iwezekanavyo.

"Niwaagize maofisa elimu wote wa wilaya, kuhakikisha kila wanafunzi wawili wanakabidhiwa mti mmoja wauhudumie kwa muda wao wote watakaokuwa masomoni.

Haiwezekani wanafunzi wawili wakabidhiwe mti mmoja, halafu washindwe kuuhudumia. Utakuwa ni uzembe katika usimamizi," alisema Mongela.

Hali kadhalika Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha, Suleyman Msumi, akiwa ndiye mwenyeji wa shughuli hiyo, aliahidi utekelezaji wa maagizo hayo ya mkuu wa mkoa ambayo yametokana na maelekezo ya Waziri Mkuu, Makamu wa Rais pamoja na waziri mwenye dhamana ya mazingira kwamba katika shule na taasisi mbalimbali, ipandwe miti ya matunda ambayo itakuwa na faida nyingi, moja ikiwa kupata matunda, kivuli lakini pia hewa safi lengo likiwa ni kutokomeza jangwa.

Alisema kampeni hiyo lengo lake haswa ni kutokomeza jangwa, kutokomezwa hali ya ukame na kupambana na uharibifu wa mazingira, suala ambalo linasababisha mabadiliko ya tabianchi, hivyo kuhakikisha kila kaya, kila mwanafunzi, kila taasisi na asasi zisizo za kiserikali zinapanda miti lishe pamoja na ile ya mbao.

Maoni yangu ni kwamba kwa hali ya dunia ilivyo sasa, tuna kila sababu ya kuchukua hatua kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Leo ni Aprili, mwezi ambao kwa hali ilivyokuwa zamani, tungekuwa kwenye kipindi cha mvua nyingi za masika lakini sisi sote ni mashahidi kwamba maeneo mengi nchini hakuna mvua inanyesha.

Hii ni hatari sana kwa maisha yetu maana tukishindwa kuzalisha chakula cha kutosha, hali ya maisha yetu inakuwa ngumu maradufu kadri siku zinavyokwenda.

Tutakumbuka miaka ya nyuma wakati ambao bado eneo letu la nchi lilipokuwa limejawa na misitu ya kutosha, mvua zilikuwa nyingi, hivyo suala la upatikanaji wa chakula halikuwa tatizo.

Mabadiliko ya tabianchi yanasababisha matatizo makubwa sana ya kijamii. Nakumbuka wakati huo, vyakula vilipatikana kwa wingi, hivyo kwenye familia zetu tuliishi na watu ambao hawakuwa ndugu zetu wa damu kwa sababu hatukuwa na shida ya vyakula.

Leo inakuwa ngumu hata ndugu kuishi kwa ndugu kwa sababu uzalishaji wa chakula umekuwa duni kwa hiyo tunashindwa kuishi na watu nyumbani kuogopa bajeti.

Nakubali kwamba ongezeka la watu linasababisha uharibifu wa mazingira kwa maana misitu hufyekwa kwa ajili ya makazi. Lakini bado tunayo nafasi ya kuyafanya maeneo yanayostahili kupandwa miti yapandwe ili kukabiliana na tatizo la ukame.

Ziko nchi Afrika Mashariki watu wameanza kufa kutokana na njaa kwa sababu nchi zao zimegeuka na kuwa majangwa, hivyo hawazalishi chochote.

Kwa hiyo kama tutaendelea kukata miti bila kupanda, hatutakuwa tumebarikiwa sana zaidi yao maana yake matatizo yanayowapata leo yatatupata sisi kesho, kwa hiyo ni suala la muda tu.

Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) limeripoti vifo vya watoto na mifugo katika eneo la Somaliland kutokana na ukame wa zaidi ya miaka miwili sasa.

Maana yake ni kwamba nchi imeshageuka kuwa jangwa kwa hiyo ni muhimu Watanzania kutosubiri hali iwe hivyo badala yake tuhamasishane kupanda miti kwa wingi ili kulinda uoto wetu wa asili.

Jambo hili si la viongozi tu pekee kwa sababu suala la utunzaji wa mazingira ni uhai wa kila mmoja wetu.

Pengine tunaweza tusielewe kwa urahisi faida za kupanda miti ambazo nje ya miti kutumika kama matunda, kuhifadhi vyanzo vya maji, kuvuta mvua, kuwa makazi ya viumbe wengine, kutoa nishati ya mkaa na kuni, kufanya mazingira yapendeze, kutoa kivuli lakini kazi kubwa ya miti pia ni pamoja na kunyonya na kuhifadhi hewa ya ukaa, ambayo inatokana na shughuli za binadamu kama viwanda na upikiaji wa kuni.

Hewa ya ukaa isiponyonywa na kuhifadhiwa na mimea hutoboa Ozoni (O3) ambayo kazi yake kubwa ni kufyonza na kutukinga na mionzi mikali ya jua.

Hali hiyo isipozuiwa, inasababisha ongezeko la joto na maradhi ya saratani ya ngozi kwa binadamu na viumbe wengine.

Tumesikia pia kupitia vyombo vya habari vifo vya watu vilivyosababishwa na ongezeko la joto kwenye nchi zao.

Hiyo ni moja ya madhara ya kuharibika kwa Ozoni, hivyo mionzi inapiga moja kwa moja. Lakini wimbi la watu kuugua saratani sisi ni mashahidi hapa nakadhalika.

Kwa hakika hakuna maisha bila miti, kwa sababu miti huzalisha hewa ya Oksijeni kwa hiyo ni ukweli uliowazi kwamba hakuna miongoni mwetu anayeweza kuishi bila kuvuta hewa ya hiyo.

Kwahiyo ili tuweze kupata hewa safi duniani, lazima tupande miti kwa wingi.

Rai yangu kwa wataalamu wa misitu kwa kushirikiana na serikali, oneni umuhimu wa kuotesha miti mingi kwenye viriba kama mbegu ili taasisi za serikali kama shule, taasisi binafsi pamoja na watu binafsi wakabidhiwe bure. Wasimamiwe kuhakikisha inapandwa na kukuzwa.

Pengine nishauri viundwe vikosi kazi katika kila wilaya vya kuhakikisha miti inapandwa na inakua vyema. Hali halisi tunaiona kila kona ya nchi watu tunalia juu ya ongezeka la joto, sasa dawa yake tupande miti kwa wingi ili pia mvua ziwe zinanyesha kwa mpangilio kuliko hali ilivyo sasa, kwamba wakati wa masika hakuna mvua wakati wa kiangazi ndiyo mvua zinanyesha. Hii yote ni kutokana na uharibifu wa mazingira. Tuyatunze mazingira yatutunze.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

### BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# 'Georgina' na 'Rangi ya Chungwa' nyimbo zisizochuja wakati wote



Na Adam Fungamwango

**'Georgina' na 'Rangi ya Chungwa' zilitungwa na kurekodiwa mwanzoni kabisa mwa miaka ya 1970 na bendi mbili ambazo hazikuwa kubwa sana, lakini zikawa maarufu zaidi kuliko hata bendi zenyewe.**

HADI leo mwaka 2022, ukienda kwenye bendi yoyote inayopiga muziki 'laivu', haitamaliza onyesho lake kabla hazijapigwa nyimbo mbili maarufu sana. Nyimbo hizo ni 'Georgina' na 'Rangi ya Chungwa'.

Hata kama wanamuziki wenyewe hawakuwa na mpango nazo kuzipiga, yatapelekwa maombi jukwaani kutoka kwa wapenzi wa muziki waliofika hapo kuburudika ili zipigwe. Wako wenye umri mkubwa wanaoomba, lakini kuna wakati utashangaa kuona zinaombwa na vijana wenye umri hata wa miaka 20, wavulana kwa wasichana.

Kitakachokushangaza zaidi, nyimbo hizo zinapopigwa, vijana wenye umri wa kuanzia miaka 20 hadi 30, wanaziimba kwa kufuatisha maneno vile vile. Utafikiri ni nyimbo mpya zilizorekodiwa miaka ya 2000 kumbe ni za kitambo kabla hata hawajazaliwa na pengine baadhi yao wazazi wao walikuwa bado makinda au hawajazaliwa wakati zilipotungwa.

Mbali na kuimba mashairi neno kwa neno, huimba kwa hisia kali, huku wakicheza na kuonyesha kabisa si tu kwamba wanaburudika na muziki 'laivu' tu bali hata , lakini hata maudhui ya nyimbo hizo yanawaingia moyoni.

Ni kweli nyimbo nyingi za zamani za dansi zimeendelea kupendwa na mashabiki wengi wa muziki na kuzipachika majina ya 'muziki usiokufa'. Lakini nyimbo hizi mbili ndizo zimekuwa kama vinara wa nyimbo zote za zamani kwa kupendwa.

'Georgina' na 'Rangi ya Chungwa' zilitungwa na kurekodiwa mwanzoni kabisa mwa miaka ya 1970 na bendi mbili ambazo hazikuwa kubwa sana, lakini zikawa maarufu zaidi kuliko hata bendi zenyewe. Hata hawa vijana wa sasa ambao wanazipenda nyimbo hizi, pamoja na kuziimba kana kwamba ni za 'bongo fleva', wengi hawajui zimepigwa bendi gani.

Mmoja anaweza kutokea akasema ni Marijani Rajabu aliyeimba 'Georgina'. Sawa, atakuwa yuko sahihi. Wimbo huu ulipigwa na bendi ya Safari Trippers, ukiimbwa na Marijani, lakini ulitungwa na Khalfan Uvuruge.

Kisa cha wimbo huu ni cha kweli na msichana huyo Georgina alikuwepo. Ni kwamba wanamuziki wa bendi hiyo walipokuwa wakitoka mazoezini siku moja walikwenda kwenye nyumba moja wakagonga hodi wakaomba maji ya kunywa. Kumbuka zamani hakukuwepo maji ya chupa madukani na ulikuwa utaratibu wa kawaida zamani kwa mtu kuomba maji ya kunywa kwenye nyumba yoyote ile njiani hata kama huijui na hawakujui, lakini utapewa tu.

Msichana Georgina ndiye aliyewapa maji na Uvuruge alivutiwa naye, uhusiano ukaanzia hapo. Baba mtu akatonywa kuwa binti yake ambaye ni mwanafunzi wa sekondari wakati huo ana uhusiano na vijana wa bendi inayofanya mazoezi jirani ya nyumbani kwake.

Alichofanya mzee akamhamisha shule kumpeleka mikoani, ndipo Uvuruge alipotunga wimbo huo.

"Oooh Georgina, siku uliyoondoka, uliniacha nalia na machozi, umekwenda kuishi mbali nami, Georgina ya mama aaah. Sipati Usingizi nikikumbuka, tulivyoishi mimi nawe Georgina aaah, ooh Georgina. Umeondoka Georgina, umeniachia masikitiko, Georgina Georgina ooo." Hayo ni baadhi tu ya maneno yaliyo kwenye wimbo huo.

Nyanyembe Jazz, si bendi inayojulikana na wala haikuwa bendi kubwa wakati huo. Pia bendi hiyo iliyokuwa chini ya Kassim Mponda, haina nyimbo nyingi maarufu. 'Rangi ya Chungwa' ndio wimbo wake maarufu zaidi kuliko bendi yenyewe hadi leo hii.

Awali uliitwa 'Rangi ya Fanta' na msichana aliyeimbwa alisifiwa kuwa ana rangi ya fanta. Kamati ya Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD), iliwaambia kama haina makubaliano ya kimkataba na wahusika na kampuni ya vinywaji wabadilishe. Ndipo walipobadilisha baadhi ya maneno, ikiwemo sasa kuwa 'Rangi ya Chungwa'.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya siri-26

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

HAIKUISHIA hapo. Eddy alidakwa na watu viongozi wa mashirika yasiyo ya kiserikali, yanayodili na unyanyasaji wa kijinsia, na hasa wasichana wadogo. Mengine yalikuwa ni ya kuwasaidia wasichana wanaofanya kazi za ndani ambao walionekana kuguswa na kesi hiyo.

Eddy alionekana kushangaa, kwa sababu yeye hakuwa wakili kwenye kesi hiyo, na wala hakusimama mahakamani. Alichofanya ni kupeleleza, na hakuna mtu aliyemuona. Alifanya kazi yake peke yake, hadi alipokamilisha na kumkabidhi Tinga.

Alimwita Tinga. "Hebu wajibu maswali yao, mimi sihusiki na maswali haya." Alijitoa.

Ni kama vile tayari walishajua mtu aliyekusanya upelelezi wote mgumu, uliokuwa umejifungafunga na kuuweka wazi ni yeye.

Ndiyo maana alikwenda kujibu chochote. Hakutakiwa kufanya hivyo. Ndiyo maana alimpa kazi hiyo Tinga.

"Ongea nao hawa viongozi wa mashirika yasiyo ya kiserikali, pamoja na wanahabari, wana maswali wanataka kukuuliza, wewe kama wakili wa kesi hii unaweza ukawa mtu sahihi zaidi, mimi ngoja nikapumzike, tutawasiliana kesho." Alisema Eddy akamshika mkono mpenzi wake na kuingia kwenye gari.

***********************************

Usiku wa deni hauchelewi kucha. Siku ya hukumu ilifika. Mahakama ya Rufaa haikujaa, ila ilifurika.

Ilifurika watu na magari pia. Ilifurika watu wenye nyadhifa kubwa, wasomi na raia wa kawaida. Magazeti, mitandao ya kijamii, redio vyote vilitumika kuitangaza sana kesi hiyo ya aina yake. Tena waliianza tangu ilipoendeshwa kwa mara ya kwanza na hukumu ya kunyongwa na Tina Kauzeni, ambaye alisubiri utekelezaji wa hukumu hiyo kwa miezi sita, kabla ya kuanza kusilizwa kwa rufaa.

Kisa hicho kama filamu au tamthilia ya kusikitika, iliwafanya watu wengi ambao hawahusiki hata chembe na hukumu hiyo kuwa wengi zaidi kuliko wahusika wenyewe.




**Msichana ambaye hata yeye alifahamu kuwa ndiye muuaji halisi. "Vielelezo vilivyoletwa hapa vinaonyesha kuwa mke wa marehemu alifanya mauaji haya akishirikiana na mtu huyo, ambaye inaonyesha wana uhusiano wa kimapenzi.**

Kila mmoja alichukua nafasi yake, Jaji Pius Msemwa ambaye yeye ndiyo huongea kwa niaba ya wenzake, Edson Njau na Shaaban Jeje, alisimama.

Kila mmoja alibaki kimya. Hakuna hata aliyekohoa. Unaweza hata ukaangusha sindano ukaisikia.

"Leo hii tutatoa hukumu ya kesi ya mauaji yanayomkabili Tina Kauzeni ambaye alihukumiwa na Mahakama Kuu kwa kosa la kumuua bosi wake. Au baba mwenye nyumba, Hafidh Chilambo. Mtuhumiwa anadaiwa kumuua kwa kumuwekea aina mbili za dawa alizozinunua kwenye duka la dawa na kumuwekea kwenye chakula. Mtuhumiwa alihukumiwa kunyongwa hadi kufa. Baada ya miezi sita, kesi hii ikaletwa kwenye Mahakama ya Rufaa ili hukumu kupitiwa upya.

Upande wa mashahidi hawakuleta ushahidi wowote zaidi ya ule wa kwanza. Upande wa utetezi ambao ulikata rufaa ukaleta ushahidi wake hapa. Tumepitia ushahidi na vielelezo vya pande zote mbili. Baada ya hapo jopo letu likakaa na kuamua kutoa hukumu hapa leo, kulingana na ushahidi wa pande zote mbili jinsi ulivyokuwa.

"Mahakama imekubaliana na pande zote kuwa ni kweli mtuhumiwa alikwenda kununua dawa hizo ambazo zikiwekwa kwenye chakula zinageuka kuwa sumu. Lakini imekubaliana na upande wa utetezi kuwa mtuhumiwa hakufika nazo nyumbani, kwani alipofika njiani alikutana na Abdallaah Mtola aliyekuwa akiendesha gari aina ya Toyota Alphard. Ushahidi usio na shaka umeletwa hapa.

Pia imejidhihirisha kuwa huyo mtu alikutana kwa siri na mke wa marehemu, kabla ya mtuhumiwa kufika nyumbani na kumkabidhi kifuko cha dawa.

Mahakama imekubaliana na upande wa utetezi kuwa ni kweli mke wa marehemu ambaye aliondoka asubuhi hiyo na watoto wake Temeke kwa shangazi yake alirejea, ushahidi wote uko wazi, akajificha ndani chumbani kwake na kujifungia mlango kwa ndani." Hapo tu tayari kila mmoja alianza kushuku jambo kwenye kesi hiyo.

"Mahakama imepata na kukubaliana na ushahidi kuwa mke wa marehemu alijifungia humu kwa nia ovu. Alimsubiri mtuhumiwa apike chakula na alipomaliza, tayari alishapanga mkakati wake mapema, kwani alishampa pesa tangu jana yake kuwa mchana aondoke kwenda Ilala kununua nguo. Yaani kama alimpa zawadi. Lakini aliuhitaji huo muda. Baada ya mtuhumiwa kuondoka akiwa hajui kuwa mama yumo ndani, mke wa marehemu alitia dawa hizo alizopewa na Mtola kwenye chakula cha mumewe na baada ya kufanikiwa hilo, alitoka na kumuonya mlinzi asiseme lolote lile. Na ndiyo jambo lililosababisha aachishwe kazi, na kupewa pesa nyingi, kwani waliopo kuna siku siri inaweza kufichuka.

Mahakama inaamini kuwa jambo hilo liliandaliwa kwa muda mrefu na kwa umakini mkubwa, kwani mke wa marehemu na mshirika mwenzake aliyetajwa kortini kwa jina la Mtola, walifanya makusudi ili mtuhumiwa aonekane kuwa muuaji, iwe salama kwao. Ndiyo maana walimtuma hizo dawa na hawakutaka zifike nyumbani kwa sababu itaonekana kama zilifika, basi yeyote yule anaweza kuhisiwa kufanya kutendo hicho. Na ililengwa mke wa marehemu asihisiwe kwa lolote lile, ndiyo maana hata mauaji yalipangwa siku ambayo ndugu yake mmoja alikuwa na sherehe za harusi. Ikapangwa kuwa siku hiyo iwe siku ya mauaji. Kwa sababu ilionekane alikuwa hayupo kwa siku nzima. Na hilo lilifanikiwa kwani, ndiyo msingi mzima wa hukumu ya kwanza ilikolalia.

Mahakama pia imekubaliana na upande wa utetezi kuwa mtuhumiwa hakujua chochote kile kinachoendelea, kwani baada ya kukabidhi dawa, alirudi nyumbani kupika chakula cha marehemu, na kwa bahati nzuri mara baada ya kupika alikipakua na kukiweka kwenye 'poti', kabla ya kuondoka kwenda kununua nguo Ilala, hivyo mke wa marehemu aliweka mchanganyiko huo wa dawa iliyogeuka kuwa sumu kwenye mchuzi na chakula kidogo ambacho ni wali. Hakuweka kwenye chakula chote kilichopikwa, kwani ingeweza kusababisha hata kifo cha mtuhumiwa mwenyewe."

Umati ulikuwa kimya. Wengine walibaki midomo wazi wasiamini kile kinachotoka kwenye kinywa cha Jaji huyo. Baadhi ya akinamama walianza kububujikwa machozi kimya kimya.

"Mtuhumiwa huyu huyu ambaye alihukumiwa kunyongwa. Leo kibao kinaonekana kugeuka. Ni ajabu na kweli." Mwahija ambaye alikuja mara ya kwanza kutoa ushahidi wa kumuuzia dawa. Alichokisikia hapo hakuamini masikio yake. Naye machozi yalianza kumbubujika kama bomba la mvua. Msichana ambaye mara kwa mara alikuwa anakuja kwenye duka na kumuuzia dawa. Msichana ambaye hata yeye alifahamu kuwa ndiye muuaji halisi.

ITAENDELEA JUMAPILI



## SIRI NZITO YA MAUNDA

# Baba yake asema kila kitu kwa uchungu

BABA Mzazi wa marehemu Maunda Zorro, Mzee Zahir Zorro ametoboa siri ambazo wengi walikuwa hawazifahamu kuhusu msanii huyo.

Maunda alifariki usiku wa kuamkia Alhamisi katika ajali ya gari iliyotokea Kigamboni na mazishi yake yalifanyika jana nyumbani kwake Kongowe jijini Dar es Salaam.

Mzee Zorro, amesema baadhi ya mambo aliyokuwa nayo binti yake ni kufanya mambo magumu kiasi ambacho wakati mwingine anamsahau kama ni mtoto wa kike.

Amesema kabla Maunda hajapata watoto, alikuwa anasahau kama ni mwanamke kwa sababu alimfundisha mchezo wa mapigano ya Martial Arts baada ya kutoka jeshini.

"Nilikuwa nasahau kuwa ni mwanamke, najua ni mtoto wangu wa kiume, lakini yeye ananikumbusha kuwa ni msichana" amesema Zahir Zorro.

Mzee Zorro amesema kitu kingine ambacho watu hawakifahamu ni uwezo wake wa kuimba kwa nguvu na sauti yake nzito, pia huimba akiwa na furaha tu na asipokuwa na furaha hawezi.

Amesema jambo lingine ni kwamba Maunda aliamua kuacha muziki ili apate nafasi ya kupata watoto na katika maisha yake alifanikiwa kupata watoto watatu kwa wanaume wawili tofauti.

Aidha, msanii huyo alikuwa na tabia ya kuamka akiwa amekasirika bila sababu yoyote, lakini alikuja kubadilika baada ya kupata watoto wake ambao walikuwa wakimuuliza mara kwa mara kwa nini anakuwa katika hali hiyo.

Mzee Zorro amesema mwanawe alilazimishwa kuanguka kisanii kutokana na kadhia iliyopo katika sekta ya muziki ambayo wanapokuja wasanii wapya wale wa zamani wanapotezwa kwa lazima.

"Kadhia hii ipo sana hapa Tanzania, endapo msanii mpya akiibuka wale wa zamani wanalazimishwa kupotea, hali hii ilimkumba mwanangu na bado inaendelea kuwatokea wengine," ameongeza kusema.

# Rich Omytz awachana mastaa Bongo

Msanii wa Bongo Fleva mwenye makazi yake Afrika Kusini, Rich Omytz, amewataka mastaa wa Kitanzania kupunguza maringo kwa wasanii wachanga.

Akizungumza na Nipashe, Rich Omytz ambaye anatamba na ngoma yake mpya inayoitwa 'Zigo', amesema kuna mwanamuziki mkubwa wa Bongo aliwahi kumuonyeshea dharau pale alipomwomba kolabo wakati alipokwenda ,Afrika Kusini.

"Wasanii tunategemeana kuna msanii mkubwa alikuja hapa Cape Town, nikamtafuta ili tufanye kolabo lakini hakuonyesha ushirikiano kabisa kama vile hanijui, hilo jambo liliniumiza sana ingawa sikukata tamaa mpaka nimeachia video ya Zigo," amesema Rich.



## ZISIKUPITE

### NUNEZ ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle imetoa kwa Benfica euro pauni milioni 60 kwa mshambuliaji wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22. ***(Footmercato)***

### SARRI AMTAKA JORGINHO

KOCHA Maurizio Sarri anatamani kuungana tena na Jorginho kule Lazio, huku kiungo huyo wa kati wa Italia mwenye umri wa miaka 30, akiwa hana uwezekano wa kupewa mkataba mpya na Chelsea baada ya 2023. ***(90min)***

### TCHOUAMENI ATAKIWA NA HAG

KOCHA anayekuja wa Manchester United, Erik ten Hag anamtaka kiungo wa kati wa Monaco na Ufaransa, Aurelien Tchouameni na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 anapendelea kuondoka Ligue 1. ***(ESPN)***

### GRILLITSCH AWANIWA

ARSENAL wana nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Hoffenheim na Austria, Florian Grillitsch mwenye umri wa miaka 26, kwa uhamisho wa bure msimu huu wa joto. ***(Telegraph, via Metro)***

### NEVES ATAKIWA ARSENAL

KIUNGO wa Wolves na Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25, anawaniwa na Arsenal. ***(Sky Sports)***

### LEWANDOWSKI NA BARCA

STRAIKA wa Poland, Robert Lewandowski anapanga kuondoka Bayern Munich kipindi cha majira ya joto na ameshafikia makubaliano binafsi na Barcelona. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 mkataba wake na Bayern unamalizika kipindi ch majira ya joto 2023. ***(TVP Sport, via Mail)***

### MERINO HUYO MAN

KLABU ya Manchester City inawania kumsajili nyota wa Real Sociedad, Mikel Merino mwenye umri wa miaka 25 ambaye ada yake ni pauni milioni 50. ***(El Confidencial, via Manchester Evening News)***

### FERNANDEZ ATAKIWA CITY

PEP Guardiola pia anamtaka kiungo wa River Plate, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 21 kwenye kikosi chake. ***(Goal)***

### KULUSEVSKI KUBAKI SPURS

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte anataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu kiungo wa Sweden, Dejan Kulusevski mwenye umri wa miaka 21 ambaye anacheza kwa mkopo kutoka Juventus. ***(Calciomercato)***

### YILMAZ ATAKIWA

MLINZI wa kushoto wa Besiktas, Ridvan Yilmaz mwenye umri wa miaka 20 anawaniwa na Leicester City. ***(TGRT Haber)***

### NUNEZ KUONDOKA

STRAIKA wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22, ataondoka Benfica kipindi cha majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# PARTEY NJE HADI MWISHO WA MSIMU

**Ni kutokana na jeraha la paja na hivyo hatarudi uwanjani hadi msimu ujao na...**

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amekiri kwamba Arsenal wanatarajia kumkosa kiungo, Thomas Partey kwa muda uliobaki wa msimu huu.

**Partey alipata jeraha la paja wakati wa kichapo cha 3-0 kutoka kwa Crystal Palace mapema mwezi huu na alitarajiwa kukosa angalau wiki chache, lakini sasa atakuwa nje ya uwanja kwa muda wote uliobaki.**

"Habari tulizopata baada ya kufanyiwa tathmini sio nzuri," alisema Arteta.

"Haionekani kuwa chanya sana kwa yeye kurudi uwanjani msimu huu, lakini itabidi tusubiri na kuona. Anajaribu kurejea haraka iwezekanavyo lakini kwa sasa hatuna matumaini makubwa kuhusu hilo.

"Wakati huu sio mzuri. Tulijua kuelekea mwisho wa msimu moja ya vipengele muhimu itakuwa kuwa na timu inapatikana kwa kadri iwezekanavyo. Tuna masuala machache naye na (Takehiro) Tomiyasu, lakini inabidi tuendelee kushindana."

Partey alikuwa katika hali nzuri kabla ya jeraha lake lakini kama ilivyo kwa mlinzi wa kushoto Kieran Tierney, Arteta lazima atafute njia ya kustahimili hali hiyo bila yeye.

Arteta alikuwa na habari njema kuhusu mshambuliaji Alexandre Lacazette, ambaye alikosa mazoezi mapema wiki hii. Uvumi ulienea juu ya kwanini Mfaransa huyo hakuwepo, na wakati Arteta alikataa kutoa maelezo, Lacazette alitarajiwa kusafiri na Arsenal kwenda Southampton jana Jumamosi.

"Ni wazi, kuna sababu za kibinafsi ambazo siwezi kuzungumzia lakini sina habari za timu nyingine za kutoa isipokuwa vijana ambao tumejadiliana," Arteta alisema.

"Tutaona kama anapatikana. Kuna uwezekano mkubwa kuwa ndivyo hivyo."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
SEVILLA FC
VERSUS
REAL MADRID
1 | 2.86
X | 3.20
2 | 2.52

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: SALAH ATAMALIZA MSIMU IMARA




**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesisitiza kuwa nyota, Mohamed Salah atamaliza msimu akiwa imara baada ya kupunguziwa dakika kwa hivi karibuni.

Salah, ambaye ana mabao 28 katika mechi 40 za klabu kwenye michuano yote msimu huu, amecheza dakika 90 pekee mara moja tangu Liverpool ilipopoteza nyumbani kwa Inter Milan, Machi 8 mwaka huu.

Fowadi huyo wa Misri aliiongoza nchi yake kumaliza katika nafasi ya pili kwenye Kombe la Mataifa ya Afrika Januari, lakini hajaifungia Liverpool bao tangu Februari 23.


Lakini Klopp hana wasiwasi kuhusu utayari wa nyota wake, akionesha uzito wa ratiba yake ya hivi majuzi.

"Najua kuwa Mo atamaliza kwa nguvu," alisema. "Na kwa sasa tunapaswa kuweka upya kwa sababu kila mchezo kwetu ni fainali. Tangu mwanzoni mwa Januari.

"Tatizo tulilonalo ni kwamba Januari alikuwa na kipindi kikali zaidi katika maisha yake yote. "Walicheza fainali (Kombe la Mataifa ya Afrika), walikuwa na dakika zote 120, jukumu alilonalo ni kubwa sana.

"Kuna jukumu kubwa kwenye mabega yake na mikutano ya chumba cha kubadilishia nguo na mambo kama haya bila kupona hata kidogo."

Salah alicheza dakika zote 90 mara ya mwisho dhidi ya Manchester City, wakati wakitoka sare ya 2-2.



## Matic athibitisha kuondoka Man U

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Nemanja Matic amethibitisha kuwa ataondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu.

"Baada ya kufikiria sana, nimeamua kuwa msimu huu utakuwa wa mwisho kwangu na Manchester United," amesema Mserbia huyo kupitia ukurasa wa Instagram.

"Nimeiarifu bodi, meneja na wachezaji kuhusu uamuzi wangu.

"Imekuwa heshima kubwa na bahati nzuri kuichezea klabu hii kubwa. Asante sana mashabiki kwa sapoti yao isiyoyumba.

"Sasa nitatoa kila kitu hadi mwisho wa msimu kusaidia wachezaji wenzangu kumaliza kwa nguvu iwezekanavyo. Na United ilionesha kukubaliana na mchezaji huyo na ikatoa taarifa fupi ya kumshukuru.

"Asante kwa juhudi zako zote katika misimu mitano iliyopita Nemanja na huu ndio mwisho wako mzuri wa kukaa United, katika wiki zijazo," ilisema taarifa ya Man United.

Matic alijiunga na United akitokea Chelsea mwaka 2017 wakati Jose Mourinho alipokuwa Old Trafford na ameichezea klabu hiyo mechi 183 katika mashindano yote hadi sasa.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# FEITOTO AIKUNIA KICHWA SIMBA SC

**Na Dennis Fussi**

KIUNGO wa Yanga, Feisal Salum 'Feitoto' amesema kwa sasa afya yake inaendelea vizuri na ataichezea timu yake kwenye mchezo wa Aprili 30 Ligi Kuu Tanzania Bara, dhidi ya watani zao Simba.

Kiungo huyo ambaye yupo kwao Zanzibar akiendelea na matibabu, amesema kila kitu kinaenda vizuri na mbali ya kuendelea na tiba, lakini ameshaanza mazoezi mepesi ikiwemo kukimbia ufukweni mwa bahari.

**"Namshukuru Mungu afya yangu inaendelea kuimarika, yale maumivu niliyokuwa nikiyasikia hivi sasa yamepotea na tayari nimeanza mazoezi mepesi, naamini hadi kufikia siku ya mchezo wetu na Simba nitakuwa tayari," amesema Feisal.**

Amesema binafsi ameupania mchezo huo, sababu anaamini ndio umeshikilia hatma yao ya ubingwa, ndio maana anataka kuwa sehemu ya mchezo, ili kuingia kwenye kumbukumbu ya klabu hiyo.

Amesema anafurahishwa na mwenendo wa timu yake katika mechi kadhaa walizocheza hivi karibuni, ambazo walishinda.

Feisal amesema hiyo imeonesha namna walivyodhamiria kulisaka taji hilo msimu huu, baada ya kumaliza misimu minne bila kuambulia chochote.



Kocha wa timu ya mpira wa Kikapu ya JMK, Konnel Owiso, akizungumza na wachezaji wa timu hiyo wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Ruvu Shooting yaipeleka Yanga Kigoma*

**Na Adam Fungamwango**

MECHI ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Ruvu Shooting dhidi ya Yanga itapigwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma Mei 4 mwaka huu.

Msemaji wa klabu ya Ruvu Shooting, Masau Bwire amesema kuwa wameamua kuipeleka mechi hiyo baada ya kukamilisha taratibu zote za kikanuni na kuwa wao ndiyo wenyeji wa mchezo huo.

"Tunapenda Watanzania wapate burudani, tumeamua kusambaza mechi zetu ili ziwafikie mashabiki wote nchini. Tulipata maombi kutoka sehemu mbalimbali, Tabora, Songea, Mwanza na Arusha, kote walitaka mechi yetu ipelekwe huko, lakini tukaona sehemu ambayo hatujawahi kufika kabisa ni Kigoma ambako nako tuliombwa, kwa hiyo tukaamua tupeleke huko. Ukweli ni kwamba mechi yetu ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga tumeipeleka kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika na tutacheza huko, Mei 4 mwaka huu. Tunawahakikishia tu mashabiki kuwa tutacheza soka safi na Mungu akipenda kushinda mechi," alisema Masau.

Imekuwa ni utamaduni sasa kwa timu za Ruvu Shooting na KMC kupeleka mechi zake mikoani, hasa zikicheza na timu kubwa za Simba na Yanga na zenyewe zikiwa ndiyo wenyeji wa mchezo.

Kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu dhidi ya Simba, Ruvu Shooting ikiwa mwenyeji, iliupeleka mchezo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, ambapo hata hivyo ilikubali kipigo cha mabao 3-1 Novemba 19, 2021.

Hata hivyo, baadhi ya wadadisi wa masuala ya michezo wanadai kuwa hii inatokana na timu hizo kutaka mapato ya mlangoni zaidi kuliko ushindi, kwani, wanakopeleka kuna mashabiki wengi wa timu za Simba na Yanga wanaotaka kuziangalia, lakini ni timu mwenyeji ndiyo inayochukua mapato yote ya mchezo.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 17/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3421 | Nice vs Lorient | 1.71 | 3.66 | 4.81 |
| 15:00 | 1385 | Granada vs Levante | 2.40 | 3.44 | 2.83 |
| 15:30 | 1250 | Sturm Graz vs Rapid Vienna | 1.80 | 3.50 | 3.88 |
| 15:30 | 1355 | Austria Vienna vs RB Salzburg | 5.24 | 4.17 | 1.49 |
| 16:00 | 1195 | Celtic vs Rangers | 2.21 | 3.21 | 2.97 |
| 16:00 | 1471 | Malmo vs AIK Football | 1.70 | 3.40 | 4.57 |
| 16:00 | 1662 | Metz vs Clermont Foot | 2.71 | 3.12 | 2.66 |
| 16:00 | 2924 | Nantes vs Angers | 1.94 | 3.37 | 3.97 |
| 16:00 | 3372 | Troyes vs Strasbourg | 3.67 | 3.31 | 2.04 |
| 16:00 | 3858 | Kasimpasa vs Adana Demirspor | 2.36 | 3.34 | 2.84 |
| 16:00 | 4901 | Kalmar vs Degerfors | 1.72 | 3.59 | 4.17 |
| 16:00 | 5850 | Montpellier vs Reims | 2.24 | 3.11 | 3.36 |
| 16:15 | 5154 | West Ham vs Burnley | 1.70 | 3.65 | 4.80 |
| 16:15 | 5445 | Newcastle vs Leicester | 2.20 | 3.30 | 3.20 |
| 16:30 | 1864 | Arminia Bielefeld vs Bayern Munchen | 11.96 | 6.98 | 1.19 |
| 17:00 | 1665 | Santos vs Coritiba | 1.88 | 3.16 | 3.99 |
| 17:00 | 5919 | CSKA Sofia vs Levski Sofia | 2.08 | 3.21 | 3.25 |
| 17:15 | 1423 | Atletico Madrid vs Espanyol | 1.44 | 4.42 | 7.24 |
| 18:00 | 1140 | Wolfsberger AC vs Austria Klagenfurt | 1.48 | 4.28 | 5.25 |
| 18:00 | 3605 | Viktoria Plzen vs Banik Ostrava | 1.62 | 3.94 | 5.25 |
| 18:00 | 3806 | Baumit Jablonec vs Slavia Prague | 5.85 | 3.94 | 1.57 |
| 18:00 | 5730 | Sparta Prague vs Slovacko | 1.66 | 3.94 | 4.95 |
| 18:05 | 2036 | Lyon vs Bordeaux | 1.29 | 5.61 | 8.82 |
| 18:30 | 2604 | Union Berlin vs Eintracht Frankfurt | 2.14 | 3.34 | 3.29 |
| 18:30 | 3335 | Chelsea vs Crystal Palace | 1.54 | 3.99 | 5.78 |
| 18:30 | 3765 | Sirius FK vs Helsingborg | 1.99 | 3.30 | 3.40 |
| 18:30 | 4171 | Hoffenheim vs Greuther Furth | 1.24 | 6.21 | 9.62 |
| 18:30 | 4415 | BK Hacken vs IFK Goteborg | 1.95 | 3.31 | 3.51 |
| 18:30 | 4771 | Elfsborg vs IFK Varnamo | 1.46 | 4.17 | 5.63 |
| 19:00 | 1074 | Aris Limassol vs Apoel Nicosia | 3.24 | 3.24 | 2.21 |
| 19:00 | 1981 | PSV Eindhoven vs Ajax | 3.88 | 3.50 | 1.80 |
| 19:00 | 4732 | Viborg FF vs Odense | 2.00 | 3.48 | 3.48 |
| 19:15 | 4371 | Tenerife vs Fuenlabrada | 1.62 | 3.53 | 5.57 |
| 19:15 | 5749 | Huesca vs Zaragoza | 2.01 | 3.12 | 3.81 |
| 19:30 | 4482 | Athletic Bilbao vs Celta Vigo | 1.85 | 3.48 | 4.34 |
| 19:30 | 4721 | Aris Salonica vs PAOK | 2.33 | 2.98 | 3.23 |
| 20:00 | 2516 | New York City vs Real Salt Lake | 1.59 | 4.05 | 5.46 |
| 20:00 | 3587 | Ludogorets Razgrad vs Slavia Sofia | 1.24 | 5.24 | 9.69 |
| 20:00 | 5242 | UNAM Pumas vs CF Monterrey | 2.84 | 3.18 | 2.45 |
| 20:30 | 1124 | Hapoel Beer Sheva vs Maccabi Tel Aviv | 2.78 | 3.03 | 2.44 |
| 20:30 | 4623 | CFR Cluj vs Steaua Bucuresti | 2.12 | 3.08 | 3.53 |
| 20:30 | 5265 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.95 | 3.45 | 2.26 |
| 20:30 | 5629 | Giresunspor vs Besiktas | 2.93 | 3.32 | 2.31 |
| 21:30 | 5132 | Panathinaikos vs Olympiakos | 2.93 | 3.08 | 2.45 |
| 21:45 | 5689 | Paris St Germain vs Marseille | 1.40 | 5.02 | 6.69 |
| 22:00 | 1656 | Sevilla FC vs Real Madrid | 2.86 | 3.20 | 2.52 |
| 22:00 | 2101 | Flamengo vs Sao Paulo | 1.66 | 3.66 | 4.48 |
| 22:30 | 4031 | Sporting Lisbon vs Benfica | 2.05 | 3.38 | 3.43 |
| 23:00 | 3970 | Los Angeles FC vs Sporting Kansas City | 1.58 | 4.23 | 5.24 |
| 23:00 | 5726 | Universitario vs Alianza Lima | 1.94 | 3.30 | 3.54 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Aprili 17, 2022

Nipashe




Klopp: Salah atamaliza msimu imara UKURASA 22




Mashabiki wa Simba wakiwa kwenye 'amsha amsha' wakati wa maandalizi ya mchezo wao wa leo dhidi ya Orlando Pirates wa robo fainali ya kombe la Shirikisho Afrika, CAF. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yaionya Ruvu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imeionya Ruvu Shooting kuwa pamoja na kupeleka mechi yake kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma, hakuepuki kipigo, kwani rekodi yake inaonyesaha kuwa imekuwa ikifanya vizuri zaidi ikicheza viwanja vya mikoani kuliko nyumbani.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli amesema kuwa hawawezi kutishika kwa Ruvu Shooting kupeleka mechi mkoani Kigoma na kwamba klabu ya Yanga kila mkoa kwao ni kama nyumbani, huku rekodi zikiwa zinawabeba msimu huu.

"Tumepokea barua jana (juzi) kuwa jamaa wamepeleka mechi yao Kigoma, tunawaambia wanachama na mashabiki wa Yanga wasiwe na wasiwasi, kwa sababu ipo ndani kikanuni, tutakwenda kucheza hiyo mechi, Yanga kila uwanja ni nyumbani na huwa tunapata matokeo chanya.

Sisi huwa tunapata matokeo mazuri zaidi msimu huu tukicheza nje ya uwanja wetu wa nyumbani. Ndiyo timu pekee msimu huu iliyopata matokeo mazuri zaidi ikicheza ugenini. Mpaka sasa mechi za nyumbani tumepata sare mbili, lakini mechi za ugenini tumepata sare moja na kushinda zote, kwa hiyo wala wanachama na mashabiki wasiwe na wasiwasi na hilo, tutakwenda kucheza mechi hiyo na tutawafunga kama tulivyowafunga mwanzo kwenye mzunguko wa kwanza na tulivyowafunga wengine," alisema Bumbuli.

Ruvu Shooting imeamua kuipeleka mechi yake ya Ligi Kuu dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma itakayochezwa Mei 4.

Pamoja na hayo Bumbuli amesema kuwa tayari kikosi hicho kinaendelea kujiandaa na mechi dhidi ya Namungo ambayo imepangwa kuchezwa Aprili 23 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, ikiwa ni ya mwisho kabla ya kuwavaa watani zao wa jadi Simba kwenye uwanja huo huo, Aprili 30.

# Simba kazi moja tu leo

**Na Saada Akida**

## ●●● Kocha Pablo asema wanakwenda kufanya kila jambo ambalo wanaweza, kupambana kwa ajili ya hii...

WAWAKILISHI pekee wa Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba, leo wanashuka dimbani kuivaa Orlando Pirates ya Afrika Kusini, mchezo utakaopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Simba inaingia kwenye mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 4-0, dhidi ya USGN Gendarmerie ya Niger na kutinga hatua ya robo fainali ikitokea kundi D sambamba na RS Berkane zote zikiwa na pointi 10.**

Mara ya mwisho Simba na Pirates kukutana ilikuwa mwaka 2019, walipocheza kwenye mchezo wa kirafiki ulioisha kwa sare ya 1-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco alisema wachezaji wake wako fiti na tayari kwa ajili ya kuhakikisha wanapata ushindi mnono.

Alisema mechi hiyo itakuwa ya ushindani na wanaenda kucheza kwa ajili ya kufuzu na sio kwa ajili ya kutafuta pointi kama ilivyo kwa mechi zilizopita.

"Tuko nyumbani tunatakiwa kutumia vizuri Uwanja wa nyumbani kwa ajili ya kutafuta ushindi kabla hatujaenda kukutana nao nyumbani kwao," alisema Pablo

"Mechi itakuwa ya ushindani, tumejiandaa vizuri kila kitu kinaenda vizuri, tunatambua mechi ni ngumu na tunaweheshimu wapinzani wetu na tutacheza kwa tahadhari kubwa ili kupata ushindi nyumbani," alisema Pablo.

Amewataka mashabiki wajitokeze na kujaza uwanja kwa wingi kusapoti timu yao, akiamini vijana wake wanapambana kutafuta ushindi katika mchezo huo.

Nahodha wa Simba, Shomari Kapombe alisema wamefanya maandalizi na wako tayari kukabiliana na Orlando Pirates, kuhakikisha wanashinda nyumbani.

Alisema wanaangalia mechi hiyo kwa sura tofauti kwa sababu malengo yao makubwa wanahitaji kutumia vizuri Uwanja wa nyumbani ili kufuzu na kwenda kucheza nusu fainali.

"Kwa sasa tunachoangalia zaidi ni kuhakikisha tunashinda mechi hii bila ya kujali tunashinda mabao mangapi, kwa sababu tunatakiwa kushinda mechi ya nyumbani kabla ya kwenda ugenini,".

"Kuhusu Orlando Pirates kwetu ni furaha kwa sababu Simba tunapenda kukutana na timu kubwa, hii inatoka na sisi wachezaji tunapenda kucheza mechi kubwa," alisema Kapombe.

Alisema Orlando Pirates wajiandae kwa sababu wamedhamiria kuhakikisha wanapambana kutafuta ushindi katika mchezo huo wa nyumbani.

Naye Kocha wa Orlando Pirates, Fadlu Davids alisema Simba ni timu ngumu wanapokuwa nyumbani na kuhakikisha wamejiandaa vizuri, kukabiliana na safu ya ushambuliaji ya Simba.

Alisema ameona safu ya ushambuliaji ya Simba ambao wamekuwa na kasi na tayari wamefanyia kazi ubora wa wapinzani wao katika eneo hilo.

"Tumekuja kukutana na timu nzuri, timu inapofuzu hatua hii ni lazima uipe heshima ya ubora wa wapinzani wako (Simba) hasa wanapocheza nyumbani," alisema Kocha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >